# Nipashe

Alhamisi Februari 4, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580481

www.ipp m

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710






UKURASA 11

**DK. GWAJIMA** asema pombe chanzo kikuu cha magonjwa ya akili

UKURASA 3



**ULAYA** yajivunia kuisaidia Tanzania miradi bilioni 738/-

UKURASA 3

# Mbunge CHADEMA mtegoni madai ya kura za wizi Kawe

UKURASA 2



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akishuhudia utiaji saini makubaliano ya Mradi wa Ufuaji wa Umeme kwa Nishati ya Gesi, kati ya Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Tangen, Allan Kesseler (kushoto) na Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Nishati na Madini Zanzibar, Dk. Mngereza Mzee Miraji, katika hafla iliyofanyika Ikulu, Zanzibar jana. **Habari Uk. 17.** **PICHA: IKULU**

# Hospitali zaonywa kuhusu wagonjwa shida kupumua

UKURASA 2



## RAS Arusha afariki kwa ajali ya gari

UKURASA 3

**MICHEZO** SIMBA, DODOMA JIJI HAPATOSHI UK. 24

MAONI, KATUNI UK. 6

HABARI KITAIFA

# Mbunge CHADEMA mtegoni madai ya kura za wizi Kawe

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum (CHADEMA), Felista Njau, ameingia matatani, baada ya kuibua hoja Bungeni kuhusu madai ya wizi wa kura katika Jimbo la Kawe wakati wa Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba 28, mwaka jana.

Kutokana na madai hayo, Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, amempa siku saba kupeleka ushahidi wake kwa Kamati ya Kudumu ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

Baada ya hapo, Naibu Spika amesema Bunge litatoa uamuzi wake kabla ya kuahirishwa kwa mkutano wa pili wa bunge la 12, Februari 12, mwaka huu.

Uamuzi huo wa Naibu Spika, unatokana na Mbunge wa Kawe (CCM), Josephat Gwajima, kusimama na kuomba utaratibu kwa mujibu wa Kanuni ya 70 (i), akitaka Njau alithibitishie Bunge kwamba alikamata kura maboksi 50.

Wakati anachangia mjadala wa hotuba ya Rais John Magufuli, aliyoitoa wakati wa ufunguzi wa Bunge la 12, Novemba mwaka jana, Felista Njau alisema akiwa Meneja wa Kampeni wa Halima Mdee katika Jimbo la Kawe, yeye ni kati ya watu waliokamata kura feki mabegi matano.

"Kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais, ameeleza kulinda demokrasia, uhuru, haki za wananchi na vyombo vya habari. Mpaka sasa ninavyoongea, mimi nilikuwa Meneja Kampeni wa Jimbo la Kawe wa Mheshimiwa Halima Mdee. Haki, demokrasia na usawa havikulindwa na havikulindwa tangu uchaguzi mdogo uliofanyika mwaka 2014, 2019 lakini wa mwaka 2020 ulikuwa na mambo ya ajabu.

"Mimi ni kati ya watu niliyekamata kura feki mabegi matano, lakini nikasema kwa sababu tunajua ni lazima tuseme ukweli, demokrasia tunayoiimba tuifuate kwa vitendo. Kila mtu anajua kwenye Bunge hili amekuja vipi, ameshinda vipi, kwa njia zipi.

Mbunge huyo aliendа mbali zaidi akisema kama ni haki tunaitangaza, kama ni demokrasia tunaisema, tuiishi kwa vitendo na hapa kila mtu ana imani yake kwenye Bunge hili na tusiimbe kwenye makaratasi.

Alisema kwa minajili hiyo, kuna watu, kuna wananchi waliokamatwa kupindi cha uchaguzi.

Baada ya Njau kutoa madai hayo, Gwajima alisimama akiomba utaratibu. "Nimesimama kwa Kanuni ya 70 (i) ambayo inasema mbunge hatasema taarifa ambazo hazina ukweli.

Mbunge aliyekuwa anazungumza, bahati nzuri mimi ndiye mbunge halali wa Jimbo la Kawe, niliyeshinda kwa kura 194,000 dhidi ya mpinzani wangu aliyepata kura 30,000. Mheshimiwa Naibu Spika, naomba alithibitishie Bunge lako kwamba alikamata kura maboksi 50 kama alivyosema."

Alipomaliza Gwajima kuzungumza, Naibu Spika, Dk. Tulia alisema Mbunge wa Kawe amesimama kueleza kwamba taarifa zilizokuwa zinatolewa na Njau kuhusu vitu vilivyokamatwa Kawe kipindi cha uchaguzi au siku ya uchaguzi, hazina ukweli.

"Siwezi kufahamu ukweli, anaoufahamu ukweli ni mheshimiwa Felista Njau, lakini waheshimiwa wabunge hili jengo letu hili, kuna maneno fulani hivi yanaweza kusemwa pamoja na mambo mengine kwamba hili jumba ni jumba la kisiasa, ndiyo maana wanasema mheshimiwa Spika na Bunge lako tukufu, haiyumkiniki.

"Kwamba mtu anayesimama kuchangia humu ndani, atazungumza mambo ambayo yanazungumzwa bila ushahidi, bila uhakika, kwa sababu kila mmoja wetu anaitwa mheshimiwa, ni kiongozi anayeweza kuthibitisha kile anachokisema."

Naibu Spika alimtaka Mbunge Felista kama ana uthibitisho, ataagiza apeleke uthibitisho, lakini kama hana uthibitisho, afute kauli yake kwa mujibu wa kanuni ya 70.

Baada ya ufafanuzi huo wa Dk. Tulia, Mbunge huyo (Felista), alisimama na kusisitiza ana uthibitisho na akiambiwa apeleke, atapeleka ushahidi.

Ujasiri huo wa Felista ulimfanya Naibu Spika kufafanua zaidi kuhusu uamuzi wake akisema, "Kanuni hii ya 70 inakataza Mbunge kusema uongo Bungeni na fasili ya nne, ya tano na ya sita, ukizisoma zote kwa pamoja utapata picha kwamba kiti kitaagiza Mbunge ambaye amekataa kufuta kauli kuleta ushahidi kwa kiwango cha kuridhisha Bunge na siyo kumridhisha mtu mmoja.

Alisema kwa muktadha huo, fasili ya sita inamtaka atoe muda wa kufanya hivyo.

"Kwa sababu alikamata maboksi na mabegi, hataweza kuwa nayo humu ndani maana hayatakuwa yamepita pale nje kuingia humu ndani. Kwa muktadha huo, hayo maboksi na mabegi, hayo masanduku yaliyokamatwa, naiagiza kamati yetu ya maadili itamsikiliza yeye halafu mimi nitaletewa huo ushahidi.

"Kwa hiyo mheshimiwa Njau utapeleka ushahidi wako kwenye hiyo kamati yetu na muda ninaoutoa kwa sababu leo ni siku ya Jumatano, kwa sababu ndiyo tumeanza Bunge jana kufikia Jumatano ijayo huo ushahidi uwe umeshauleta na kamati yetu ya maadili ikae wakati huo na kamati na kabla Bunge hili halijaisha tutatoa uamuzi."

## Hospitali zaonywa kuhusu wagonjwa wenye matatizo mfumo wa kupumua

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imezitaka hospitali zinazotoa huduma kwa wagonjwa zinaowapokea wenye matatizo ya mfumo wa upumuaji, kutowatoza gharama kubwa kwa sababu dalili hizo ni za magonjwa mengi na si corona peke yake.

Katibu Mkuu, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, (Idara Kuu ya Afya) Prof. Mabula Mchembe, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam baada ya kufanya ziara katika Hospitali za Aga Khan na Kairuki ili kuangalia idadi ya wagonjwa walioko huko kama wana matatizo ya upumuaji kama mitandao ya kijamii inavyodai.

Prof. Mchembe alizitaka hospitali zisitumie matatizo ya mfumo wa hewa ambayo siyo corona na kuweka gharama kubwa za matibabu wakati awali waliwahudumia kwa gharama za kawaida.

"Ninawataka wananchi wapuuze taarifa zinazoeleza kuwa hospitali zina wagonjwa wa corona. Ninawaomba wasiwe waoga kwenda hospitalini kupata huduma," alisema.

Juzi, katika mitandao ya kijamii ilisambaa taarifa iliyodaiwa ni ya Hospitali ya Kairuki ambayo ilionyesha gharama za malipo ya matibabu ya magonjwa ya mfumo wa hewa kuwa ni Sh. 600,000 kwa mgonjwa ambaye hahitaji mashine ya kumsaidia kupumua (ventilator). Pia taarifa hiyo ilidai kuwa kwa mgonjwa anayehitaji mashine ya kumsaidia kupumua, atatakiwa kulipa Sh. 850,000 kwa siku na mgonjwa au ndugu wa mgonjwa au mdhamini wa mgonjwa atatakiwa kulipa malipo ya awali ya Sh. milioni moja wakati wa kutia saini mkataba.

Akifafanua taarifa hiyo mbele ya Katibu Mkuu, Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya Kairuki, Dk. Asser Mchomvu, aliikanusha kuwa si yao.

Pia Katibu Mkuu alihoji kama hospitali hiyo ina wagonjwa wenye matatizo ya kupumua na kuelezwa kuwa hadi siku hiyo walikuwa 28.

Dk. Mukiza Ngemera wa hospitalini hapo alisema kuwa mpaka sasa hospitali ina idadi hiyo ya wagonjwa ambao bado hawajafanya vipimo kuthibitisha.

"Naomba kufafanua kidogo anaposema 'clinical diagnosis' maana yake bado hawajathibitisha na kote tunakopita kinachotajwa kwa asilimia kubwa ndicho hicho, hawa (Kairuki) wanaposema wana wagonjwa 28 maana yake ni wale wa kufikirika tu hawa wanaweza wakawa na matatizo ya mfumo wa hewa, pneumonia au kitu gani lakini bado hawajathibitisha," alisema Katibu Mkuu.

Kuhusu wagonjwa hao wanavyohudumiwa, Dk. Ngemera alisema wagonjwa hao 28 wamegawanyika katika makundi matatu, wenye dalili za awali ni 12, hali mbaya wawili na dalili za kawaida ni 14.

Alisema wenye dalili za awali na za kawaida umri wao ni kati ya miaka 35 na 72.

"Tunao wenye magonjwa mengine ambapo kati yao 28, watu 16 wana magonjwa tofauti kama kisukari, shinikizo la damu wapo wenye magonjwa ya dalili za figo na mmoja ni mjamzito," alisema.

Alisema hali zao kwa wenye magonjwa ya presha na kisukari, mmoja alikuwa hajui kama wana historia hiyo na siku hiyo (jana) ndiyo wamegundua presha yake ipo juu. "Mgonjwa ambaye amekaa sana ana wiki mbili, na kwa jana (juzi) uliwapokea wagonjwa saba kwa leo (jana) hatujapokea mgonjwa hadi sasa hivi (mchana), wengi ni wale wanaohitaji oksijeni (oxygen) na wale wanaohitaji dawa kwa ajili ya kutibu magonjwa mengine yanayowakabili, kama ni kupooza atapatiwa dawa, kama ni homa atapewa lakini lazima tufanye vipimo," alisema.

Dk. Ngemera alisema tangu wameanza kuhudumia wagonjwa hao wenye matatizo ya mfumo wa kupumua, wapo wahudumu wa afya ambao nao wanaugua. "Kutoka Januari kuna waliolazwa wawili na wapo wanaohudumiwa kama wagonjwa wa nje ambao wapo zaidi ya 10 na dalili zao ni homa, kichwa na kukohoa," alisema.

Baada ya ufafanuzi huo, Katibu Mkuu aliwaeleza kuwa si kila anayeumwa kichwa, homa na kukohoa ana corona.

"Hata mwenye anaemia (ukosefu wa damu) anaweza kupata shida ya kukohoa, misuli kuuma, mwenye mafua hivyo hivyo, mama mjamzito kwa sababu mimba imekuwa kubwa anapata shida ya kupumua, kwa sababu nafasi ya kupumulia inakuwa shida. mtu mwenye matatizo ya moyo, pumu, malaria, magonjwa ya matumbo (typhoid) naye anapata shida ya kupumua, siyo dalili zakuchukulia kwa sababu naumwa kichwa ni corona," alisisitiza.

Dk. Mchomvu alisema mgonjwa mmoja mwenye matatizo ya mfumo wa kupumua anatumia silinda hadi tano kwa siku na bima ya afya inatoa Sh. 40,000 na moja huuzwa kati ya Sh. 16,000 hadi Sh. 20,000 na kumwomba katibu Mkuu kuwasaidia kulisemea hilo.

Mkurugenzi huyo alifafanua taarifa iliyosambaa mtandaoni kuhusu gharama kwa wagonjwa wenye matatizo ya mfumo wa kupumua na kumweleza Katibu Mkuu kuwa, siyo yao na kwamba hospitali hiyo imeingia mikataba na kampuni mbalimbali za bima za afya.

"Kama ingekuwa ni ya hospitali taarifa ile lazima ingekuwa na saini yangu kama Mkurugenzi. Hivi kweli mgonjwa ameletwa hawezi kupumua utampa kweli mkataba ausaini au huduma ya kwanza?" Alihoji Dk. Mchomvu.

Naye Mganga Mkuu wa Hospitali ya Kairuki, Dk. Onesmo Kaganda, alisema walishtushwa baada ya kuiona taarifa hiyo juzi na kueleza kuwa zaidi ya asilimia 80 ya wagonjwa wanaowapokea ni wa bima za afya na kwamba kauli yao ni mgonjwa kwanza.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Huduma za Afya wa Aga Khan, Dk. Ahmed Jusabani, alipinga madai kuwa hospitali hiyo imefurika wagonjwa wa corona na kufafanua kuwa wana wagonjwa wachache wa nje na wale waliolazwa.

"Tunawaomba wagonjwa ambao wamekuwa wakifika kwenye hospitali yetu kwa ajili ya huduma mbalimbali wasisite kufika kupata huduma hizo na tunawataka waachane na uvumi kuhusu wagonjwa wa corona," alisema.

## HABARI KITAIFA

# Ajali yakatisha maisha ya RAS

**Na Allan Isack,** ARUSHA

KATIBU Tawala wa Mkoa wa Arusha, Richard Kwitega, amefariki dunia katika ajali ya gari iliyotokea katika eneo la Mdori, Babati mkoani Manyara.

Akizungumza jana na vyombo vya habari jijini hapo, Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Iddi Kimanta, alisema kiongozi huyo wa serikali alifariki dunia saa 9:50 alasiri wakati akienda Dodoma kwa shughuli za kikazi.

"Ndugu wananchi wenzangu wa Mkoa wa Arusha kwa majonzi na masikitiko makubwa, napenda kuwajulisha kuwa mwenzetu Katibu Tawala wa Mkoa, Richard Kwitega, amefariki dunia kwa ajali iliyotokea katika eneo la Mdori wilayani Babati mkoani Manyara," alisema Kimanta.

Akizungumzia chanzo cha ajali hiyo, Kimanta alisema gari la RAS, liligongana uso kwa uso na basi la abiria la Makara, lililokuwa likitoka Babati Mjini kwenda mkoani Arusha.

"RAS alikuwa anakwenda mkoani Dodoma kikazi. Alipofika eneo la Mdori, gari lake liligongana uso kwa uso na basi la Makara lililokuwa likitoka Babati kuja Arusha," alisema Kimanta.

Hata hivyo, alisema baada ya ajali hiyo kutokea, walimpeleka katika Kituo cha Afya Magugu kwa ajili ya kupata huduma za matibabu na baada ya hapo wangemwahisha katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara, Babati kwa matibabu zaidi.

"Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Katibu Tawala wa Mkoa huo na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Manyara, walifika katika eneo la tukio lilipotokea na walijaribu kuokoa uhai wake, lakini alipoteza maisha wakati akipatiwa matibabu," alisema Kimanta.

Aidha, alisema mipango ya kurudisha mwili wa marehemu jijini Arusha inaendelea pamoja na taratibu za msiba.



Mbunge wa Kilolo, mkoani Iringa, Justin Nyamoga (mwenye shati jeupe), akishirikiana na wananchi wa tarafa ya Mahenge, kusonga ugali baada ya kushiriki shughuli ya ujenzi wa shule ya sekondari ya kata na kukabidhi msaada wa mifuko 70 ya saruji kwa ajili ya kusaidia ujenzi huo, hivi karibuni. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Ulevi watajwa chanzo ugonjwa wa akili

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, ametaja vyanzo kadhaa vinavyosababisha ugonjwa wa afya ya akili, huku akiwatahadharisha Watanzania kujiepusha na matumizi ya vilevi kupita kiasi kwa kuwa yanachangia ugonjwa huo.

Dk. Gwajima aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Lucy Mayenga.

Katika swali lake, mbunge huyo alitaka kujua serikali inachukua hatua gani kusaidia watu wenye afya ya akili wanaochukulia hatua za kisheria huku hatua za kuthibitisha tatizo lao zikichukua muda mrefu.

Akijibu swali hilo, Dk. Gwajima alisema vyanzo vingine vinadhibitika kwa kuwa ni vya kawaida.

Alitaja vyanzo vingine ni sababu za kibaiolojia ambavyo ni vinasaba vya kuzaliwa navyo, ukatili na msongo wa mawazo.

"Matumizi ya pombe kupita kiasi, bangi, kama mwili wako maumbile yake yana hivyo vinasaba, utajikuta umeangukia kwenye ugonjwa wa kukosa akili. Jamii yetu huko tunakokwenda tuishi vizuri matumizi ya kila kitu ni kwa kiasi isije kusababisha huo ugonjwa," alisema.

Pia alisema vitendo vya ukatili huchangia ugonjwa wa akili.

"Ukatili ukifanyika kwa binadamu katika hatua zake zote si jambo jema. Na sisi wabunge ni mabalozi wa kukemea vitendo vya ukatili maana visije kuwapeleka watu kwenye kupata msongo na kupata ugonjwa huu wakawa hatari kwenye taifa letu na jamii yetu," alisema.

Kuhusu kukabiliana na ugumu wa maisha kunachangia hali hiyo na kuitaka jamii kuondokana na mtazamo huo.

"Hili nalo la ugumu wa maisha inabidi kukaa na jamii yetu kuelimisha ichukulie positive (chanya) na si kukaa na msongo wa mawazo, wajiepushe kufikiria na kuwaza sana kuhusu maisha yao," alisema.

Katika swali lake la Msingi, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mariam Kisangi, alitaka kujua nini chanzo cha ugonjwa huo wa tatizo la afya ya akili na serikali ina utaratibu gani wa kuwasaidia wagonjwa wenye tatizo hilo.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Godwin Mollel, alisema kitaalamu hakuna chanzo kimoja kinachosababisha ugonjwa wa afya ya akili bali ni pamoja na mjumuiko wa sababu au vichocheo ambavyo mhusika amebeba kwenye vinasaba vyake.

Dk. Mollel alisema zikikutana katika mazingira mwafaka husababisha msongo wa afya ya akili na kuzaa ugonjwa.

"Katika sababu za kibailojia, uwapo wa vinasaba katika mwili vinaongeza uwezekano wa mtu kupata ugonjwa wa afya ya akili, maradhi ya muda mrefu na matumizi ya vilevi kama bangi, pombe na aina zingine za vilevi zinaweza kuwa vichocheo hasa kwa mtu mwenye vinasaba vya uhatarishi wa ugonjwa," alieleza.

# EU yajivunia kuisaidia Tanzania bil. 738/-

**Na Salome Kitomari**

UMOJA wa Ulaya nchini umesema unajivunia kutoa zaidi ya Euro 263 (sawa na Sh. milioni 738.5) kwa ajili ya miradi ya maji na usafi wa mzingira, nishati na usafiri kwa miaka tofauti.

Akizungumza na wahariri na wakuu wa taasisi za habari nyumbani kwa Balozi wa EU nchini, Manfredo Fanti, alisema miradi hiyo imeleta mabadiliko chanya kwa Watanzania ikiwamo kuharakisha shughuli za maendeleo.

Alisema mshirika muhimu katika kutoa msaada katika maji na usafi wa mazingira na EU ilitoa Euro milioni 28 sawa na Sh. milioni 78.6 kwa ajili ya kuboresha mifumo ya maji na majitaka, uboreshaji wa mifumo midogo ya maji, kukuza usafi, kujenga uwezo na kuleta mabadiliko ya kitaasisi.

"Mradi wa kituo cha maji EU ujulikanao kama Usafi Iringa umeboresha afya na hali za usafi kwa zaidi ya watu 57,000 wa kata za Nduli, Mtwivila, Kihesa, Mkimbizi na Kitwiru pamoja na shule 60. Mradi huu umeongeza ufahamu wa watu katika kukuza tabia salama zaidi za kijamii na binafsi na kuongeza uhitaji wa huduma bora za usafi wa mazingira," alisema.

Balozi huyo alisema EU kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ujerumani walichangia Euro 51 (sawa na Sh. milioni 143.2) kupata vituo vya majisafi na usafi wa mazingira chini ya mpango wa Malengo ya Milenia ya Maendeleo.

Alisema mpango huo ulizinduliwa mwaka 2011 na kuweka kipaumbele katika uboreshaji wa upatikanaji wa maji na usafi wa mazingira katika miji ya Kigoma, Sumbawanga na Lindi na kuwezesha uhakika wa maji kwa wakazi 500,000 na huduma bora za usafi wa mazingira kwa watu 150,000.

"Chini ya mpango huu uwezo wa mamlaka za miji na majisafi na kampeni za uhamasishaji umma umeimarishwa na kuboresha mfumo wa ukusanyaji, usafishaji na usambazaji wa maji. Kigoma mtandao wa usambazaji maji umeongezeka vioski vya maji na bomba za maji kwa matumizi ya wananchi, ujenzi mpya wa uvutaji wa maji kutoka Ziwa Tanganyika unaendelea," alisema.

Balozi Fanti alisema mikoa ya Lindi na Sumbawanga visima vipya vya maji na vituo vya kusafisha maji, taka vimejengwa, viwanda vya kusafisha na kuhifadhi maji vimekamilika hivi karibuni na mtandao wa usambazaji umeboreshwa kwa kiwango kikubwa.


NEPTUNE LAW

Neptune Law Attorneys
Plot No. 31, 7th Floor
Hifadhi House (NSSF House)
Azikiwe Street/Samora Avenue,
Dar es Salaam, Tanzania
info@neptuneattorneys.com
(255) 022 211 3162

IN THE MATTER OF ARBITRATION ACT CAP 15 R.E. 2020
AND IN THE MATTER OF AN AGREEMENT TO REFER ALL DISPUTES TO ARBITRATION
NOTICE TO REFER A DISPUTE TO ARBITRATION UNDER AN AGREEMENT TO REFER DISPUTES TO ARBITRATION

BETWEEN

NAM ENTERPRISES LIMITED ... Claimant

AND

AVIC-SHANTUI TANZANIA LIMITED ... Respondent

NOTICE OF ARBITRATION

We are under the instruction of our client **NAM ENTERPRISES LIMITED** of Dar es Salaam and under the Procedural Order No. 3 of the Sole arbitrator **Advocate Madeline Charles Kimei**, MCIArb-UK dated 1st of February 2021 which requires us to notify you of the Arbitration cause that is before her and is fixed for a preliminary meeting of the parties and the sole arbitrator on the 5th day of February 2021 at 11:00 am at ***iResolve Law, 3rd Floor, Tanzanite Park, New Bagamoyo Road, Dar es Salaam***.

**THEREFORE**, treat this as a formal notice of arbitration and enter appearance on the 5th day of February 2021 at 11: 00 am at ***iResolve Law, 3rd Floor, Tanzanite Park, New Bagamoyo Road, Dar es Salaam*** for Preliminary meeting without fail. Your **FAILURE** to appear on the said date shall leave the tribunal with no option but to proceed with arbitration and make orders in your absence.

Dated on this 2nd day of **February 2021**.

NEPTUNE LAW ATTORNEYS
P. O. Box 45180
DAR-ES-SALAAM

Stephen Mosha, Advocate

cc:
Adv. Madeline Kimei, MCIArb-UK

www.neptuneattorneys.com

## HABARI KITAIFA

# Wasakwa kwa tuhuma za kulawiti mtoto

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

JESHI la Polisi Mkoa wa Kusini Pemba linawatafuta vijana wawili wakazi wa Michakaeni, Chake Chake kwa tuhuma za kumlawiti mtoto wa kiume mwenye miaka saba.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kusini Pemba, Kamishna Msaidizi (ACP) Richard Mchomvu, alisema jana kuwa baada ya jeshi hilo kupokea taarifa kutoka kwa mama mzazi wa mtoto huyo, walianza kufanya upelelezi na kuwakamata vijana watatu kati ya watano wanaotuhumiwa kufanya kitendo hicho.

Alisema sasa wanaendelea kuwatafuta vijana wawili waliobaki na baada ya uchunguzi kukamilika watafikishwa mahakamani kujibu tuhuma zinazowakabili.

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi Mchomvu alisema bado jamii haijajua umuhimu wa kumheshimu mtoto na kusababisha vitendo hivyo kuongezeka siku hadi siku.

"Matukio ya udhalilishaji yamekuwa yakiongezeka siku hadi siku kutokana na jamii bado haijaelewa umuhimu wa mtoto, hivyo ni vyema elimu ikatolewa ili kuhakikisha mtoto anaheshimiwa na kuachwa salama," alisema kamanda huyo.

Alisema Jeshi la Polisi halitomvumilia mtu yeyote atakayefanya uhalifu katika mkoa huo ikiwamo wanaowadhalilisha watoto na atakayebainika hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Mapema, mama mzazi wa mtoto huyo alisema alimgundua mwanawe amedhoofika hali ya mwili, ingawa alikuwa anakula kama kawaida.

Alisema hali hiyo ilikuwa ikiendelea kila siku na kuhisi huenda mwanawe anasumbuliwa na ugonjwa.

"Nilikuwa namuuliza unaumwa na nini, ananijibu haumwi na chochote ndipo nilipoondoa shaka ya kuwa mwanangu anaumwa," alisema mama huyo.

Januari 12, usiku, alisema alimwona mwanawe hali imezidi kuwa mbaya na kufikia kukaa upande huku akijiegemeza mito, hali ambayo alisema ilimtia wasiwasi mkubwa.

Aliongeza kuwa alimuuliza kwa mara nyingine kitu kinachomsumbua mpaka kufikia kukaa kitako upande na kumweleza kuwa kuna vijana wanamfanyia kitendo cha ulawiti.

"Nilishtuka sana nikamchukua hadi chumbani nikamvua suruali, kumwangalia tayari alikuwa wazi unamwona hadi ndani," alisema mama huyo.

Alisema baada ya hapo alimchukua na kumpeleka kwa jirani yake wa karibu na kumwelezea ile hali iliyomtokea mwanawe ambayo hakupaswa kutendewa hivyo.

"Tulimwangalia tena, jirani yangu alimwambia asukume pumzi ambapo alitoka haja kubwa ikiwa na mafunza. Kwa kweli nimeumia sana," alisema.

Mama huyo alieleza, siku ya pili walimpeleka kituo cha Mkono kwa Mkono, Chakechake, na kisha kwenda kufungua kesi kituo cha polisi.

Mama huyo alisema ilimuuma sana kuona majirani zake wanamkebehi na kusema kuwa watoto wao hawawezi kufungwa kutokana na kuwa askari mpelelezi hakuona chochote alichokitaja mtoto kwa ajili ya ushahidi.

"Hivi sasa nishaanza kutengwa, kununiwa kwa sababu nimekwenda kuwashtaki watoto wao na ukizingatia wanne wana miaka kuanzia 20 na mmoja tu ndiye mwenye miaka 16," alisema.

Alisema kilichomuumiza zaidi ni kwamba siku aliyoambiwa ashirikiane na askari mpelelezi katika kuwakamata watuhumiwa, aliporudi alimkuta mwanawe tayari ameshafanyiwa tena kitendo cha ulawiti.

Naye Diwani wa Wadi ya Tibirinzi, Chakechake, Fatma Juma Khamis, alisema alikuja mama mzazi wa mtoto huyo kumweleza kadhia iliyomkumba na alimpa ushauri na kumtaka asirudi nyuma bali akimbilie kwenye vyombo vya sheria kuripoti.

## Polisi Dar yawafungulia kesi madereva mabasi

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, limefungua jalada la kesi dhidi ya walioitisha mgomo wa madereva na wamiliki wa mabasi.

Juzi, viongozi wa madereva wa mabasi waliandaa waraka wa kuhamasisha madereva wafanye mgomo kuanzia jana.

Akizungumza juzi na chombo kimoja cha habari, Kamanda wa Kanda hiyo, Lazaro Mambosasa, alisema viongozi hao walihamasisha mgomo huo huku sababu za msingi za kufanya hivyo haziko bayana.

"Waliadhimia kwamba leo (juzi) wangegoma lakini nilitoa tamko juzi kuhusu katazo la mgomo nashukuru wameelewa na wamebadilisha nia ya kugoma sasa mabasi yote yako njiani," alisema.

Kamanda Mambosasa aliwaeleza wahusika kuwa ofisi za mamlaka zinazohusiana na masuala ya usafirishaji wa abiria ziko wazi.

"Tunawapongeza kwa kutii agizo letu lakini hatujaishia hapo tumeshaelekeza viongozi waliohusika wakamatwe wahojiwe na kuona ni hatua zipi za kisheria zitakazoweza kuchukuliwa. Tutapeleka jalada kwa Mwanasheria wa Serikali ili alipitie, walichokuwa wakikifanya ni uhuni kuhamasisha watu watende uhalifu, kuhamasisha maana yake wewe ni mshiriki wa kosa," alisema.

Kamanda Mambosasa alisisitiza kuwa kama kuna jambo lolote ambalo haliko sawa ofisi ya kanda na za usalama wa barabarani zipo wazi kusikiliza malalamiko.



Washtakiwa wa makosa matatu yakiwamo ya kupatikana na vipande 32 vya bidhaa zilizotengenezwa na meno ya tembo na tisa ya Simba, vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 45, wakiwa chini ya ulinzi wa polisi, baada ya kusomewa mashtaka yao katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mtendaji wa kijiji adaiwa kumchapa kofi mwananchi kisa kuvuta sigara

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKAZI wa Kijiji cha Mbwemkuru, Lindi mkoani hapa, Athumani Ndumba, amelalamikia kitendo cha Mtendaji wa Kijiji hicho, Azidu Mwenda, kumshambulia kwa kupigwa kofi hadharani kwa madai ya kuvuta sigara eneo la kutolea huduma za afya.

Kitendo cha kushambuliwa mwananchi huyo kinadaiwa kufanyika maeneo ya Kituo cha Afya Kitomanga, Januari 31, mwaka huu, saa 11:00 jioni na kushuhudiwa na watu waliokuwapo kusindikiza ndugu zao kupata huduma za matibabu.

Ndumba ambaye mke wake amelazwa kituoni hapo akisubiri kujifungua, alisema wakati akiwa ndani alijisikia hamu ya kuvuta sigara, hivyo akalazimika kutoka nje ili kutekeleza kile alichokikusudia.

"Mimi nilipojisikia hamu ya kuvuta sigara, nilitoka nje kutekeleza kile nilichokikusudia, na kukumbana na kadhia hii kama mlivyojionea," alisema Ndumba.

• Hata hivyo, Ndumba wakati akipewa kichapo hicho, aliendelea kutulia na waandishi walipotaka kufahamu sababu za kuwa mpole, alisema hakuwa tayari kufanya lolote kwa kuwa alikwenda kituo cha afya kwa ajili ya kumuuguza mkewe, hivyo hakuchanganya mambo na kwamba anamwachia Mungu.

Ndumba alisema baada ya kumaliza kuvuta, ndipo mtendaji huyo alijitokeza na kutaka kumfahamu mtu aliyekuwa anavuta sigara na alipojibu alijikuta akishambuliwa kwa kupigwa kofi mbili kushoto na kulia.

"Aliniita na kuniuliza nani amekuruhusu kuvuta sigara hapa? Kabla sijajibu, nikashtuka napigwa makofi mawili, moja la kushoto nikaona vimulimuli usoni," alisema.

"Kama hiyo haikutosha nikapigwa la pili, watu waliokuwa karibu nasi wakamsihi mtendaji aniache ndipo akatii na kuniacha," alisema Ndumba.

Waandishi waliokuwapo eneo hilo, walipomuuliza Mwenda, sababu za kumshambulia mwananchi huyo, alidai ni kitendo cha kukataa pale alipomuuliza mtu aliyehusika na uvutaji sigara eneo la kituo cha afya.

Alipoulizwa kama eneo hilo haruhusiwi mtu kuvuta sigara, alijibu hakuna agizo hilo ila si vizuri mtu kuvuta sigara eneo la mkusanyiko wa watu.

Sharifa Rashidi shuhuda wa kitendo cha kushambuliwa kwa Ndumba, alisema kitendo kilichofanywa na mtendaji si cha kiungwana kwa kuwa ni kinyume na taratibu za kiutumishi wa umma.

Naye Zainabu Selemani alisema sifa na matendo ya mtendaji huyo kujichukulia sheria mkononi yamekithiri kwa kuwa wiki mbili zilizopita, alimpiga na kumburuza mwana mama aitwaye Fatuma Nauchoche, pale alipomtaka kufanya ukaguzi wa usafi kwenye eneo la nyumba yake.

Pia mtendaji huyo anadaiwa kumpiga Saidi Mkuluju kwa madai ya kuchelewa kufika shuleni.

# TANGAZO

IITA
Transforming African Agriculture

ICRISAT
INTERNATIONAL CROPS RESEARCH INSTITUTE FOR THE SEMI-ARID TROPICS

## POSITION ANNOUNCEMENT

### Senior Scientific Officer - Natural Resource Management

**IITA-TZ-2021 - R4D-002 -NRS/ICRISAT-Dodoma**

The International Institute of Tropical Agriculture (IITA) on behalf of the International Crops Research Institute for the Semi – Arid Tropics (ICRISAT) invites applications for the position of **Senior Scientific Officer - Natural Resource Management.**

Background: ICRISAT is a non-profit, non-political organization that conducts agricultural research for development in Asia and sub-Saharan Africa with a wide array of partners throughout the world. ICRISAT and its partners help empower those living in the semi-arid tropics, especially smallholder farmers, to overcome poverty, hunger, malnutrition, and a degraded environment through more efficient and profitable agriculture. ICRISAT is headquartered in Patancheru near Hyderabad, India, with two regional hubs and several country offices in sub-Saharan Africa. For more details, see www.icrisat.org. AICCRA is a 3-year World Bank-funded project with ICRISAT leading the Senegal node and participating in project activities in Zambia and Kenya. ICRISAT envisions increasing access for agriculture research and extension service providers in Africa to knowledge, technologies, and decision-making tools relevant to enhancing the resilience of agriculture and food systems in the face of climate change. The project aims to implement the sub-regional component of AICCRA through building multi-actor partnerships of existing scientific and educational networks and centers to achieve outcomes by engaging with individual partners at the country level. Specifically, this project will enhance the capacity of national regional public institutions and private firms (e.g., input providers, ICT companies, media) to develop delivery models for climate services and CSA knowledge, approaches, and tools to support effective intra-regional and south-south adoption in various value chains.

**Duty Station:** The position will be based **in Dodoma** with regular travel regionally or **to Dar es Salaam**

**Essential Criteria**
- MSC degree in agriculture or related field with at least 8 to 10 years experience in national and international organizations.
- Proven expertise in implementing field programs related to research in development.
- Strong analytical and communication skills
- Fluency in English and Swahili, written and oral
- Demonstrated ability of handling multi-tasked project activities
- Willingness and physical ability to handle frequent travel to remote field sites
- Prepare clear, accurate and concise reports, records and other materials
- Ability to operate a computer using word processing, database and spreadsheet software
- Ability to collect, evaluate and interpret varied information and data

**Responsibilities**
- Provide skilled technical inputs into the planning, implementation and monitoring of demand driven agronomic and agroecological practices at on-farm study sites.
- Handle and assist the project manager in timely delivery and monitoring of field implementation and complying with reporting deadlines with partner institutes.
- Assist in organizing, facilitating meetings especially with local communities and handle the necessary logistics of training, seminars and workshops and visits of the supervisory team.
- Manage relationships with partners ensuring that field interventions are co-designed with stakeholders and interactions with communities and project partners are fair and transparent.
- Manage fund requests and disbursements of project activities, funds/grants and provide all necessary supporting documents for accounting and reporting purposes.
- Provide administrative and logistical support to project manager as well as any other project internal and external team member in the project implementation course.

**General information:**
The duration of contract for the position is one year with possible extension. This is a nationally recruited position and IITA offers a competitive remuneration package.

**Applications:** Applications including curriculum vitae, copies of certificates, telephone number, email address, and names and addresses of two referees should be sent to the Country Representative, IITA-Tanzania, Plot No. 25, Mwenge – Coca-Cola Road, Mikocheni Industrial Area P.O. Box 34441, Dar es Salaam, Tanzania or by email to **IITA-Tanzania@cgiar.org**

Applicants are requested to please indicate the reference number for the position as indicated on the heading of the announcement in your application as well as on the subject of your email if sending by email. If sending by post or hand delivery, please indicate the reference number on your application as well as on the left-hand side of your envelope. Please note that any applications without the reference number indicated will be automatically disqualified.

**Closing date:** Two weeks from the date of advertisement appearing in the newspaper.
**Please note that only shortlisted candidates will be contacted.**

IITA
Transforming African Agriculture

ICRISAT
INTERNATIONAL CROPS RESEARCH INSTITUTE FOR THE SEMI-ARID TROPICS

## POSITION ANNOUNCEMENT

### Scientific Officer (Agrometeorology)

**IITA-TZ-2021 - R4D-001 -NRS/ICRISAT-DSM**

The International Institute of Tropical Agriculture (IITA) on behalf of the International Crops Research Institute for the Semi – Arid Tropics (ICRISAT) invites applications for the position of Scientific Officer (Agrometeorology) to serve the Accelerating Impacts of CGIAR Climate Research in Africa (AICCRA) project funded by the World Bank through the CCAFS program.

**Background:** ICRISAT is a non-profit, non-political organization that conducts agricultural research for development in Asia and sub-Saharan Africa with a wide array of partners throughout the world. ICRISAT and its partners help empower those living in the semi-arid tropics, especially smallholder farmers, to overcome poverty, hunger, malnutrition, and a degraded environment through more efficient and profitable agriculture. ICRISAT is headquartered in Patancheru near Hyderabad, India, with two regional hubs and several country offices in sub-Saharan Africa. For more details, see www.icrisat.org. AICCRA is a 3-year World Bank-funded project with ICRISAT leading the Senegal node and participating in project activities in Zambia and Kenya. ICRISAT envisions increasing access for agriculture research and extension service providers in Africa to knowledge, technologies, and decision-making tools relevant to enhancing the resilience of agriculture and food systems in the face of climate change. The project aims to implement the sub-regional component of AICCRA through building multi-actor partnerships of existing scientific and educational networks and centers to achieve outcomes by engaging with individual partners at the country level. Specifically, this project will enhance the capacity of national regional public institutions and private firms (e.g., input providers, ICT companies, media) to develop delivery models for climate services and CSA knowledge, approaches, and tools to support effective intra-regional and south-south adoption in various value chains.

**Duty Station:** The position will be based Dar es Salaam , Tanzania.

**Essential Criteria**
- M.Sc. degree in Agrometeorology, mathematical or statistical sciences or a related discipline.
- Experience in climate analysis and applying crop-modelling frameworks to understanding climate risk management in agriculture.
- A deep understanding of dryland cropping systems and the application of climate services in agriculture
- Knowledge on how the application of digital agriculture and ICT may enhance productivity, logistics, or market access for smallholder farmers and value chain actors
- Experience in working with a wide range of stakeholders and interest to work in an interdisciplinary team.
- Ability and willingness to participate in fieldwork extensively

**Desirable Criteria**
- GIS and spatial analysis skills
- Experience with data visualization and design
- Experience in organizing capacity-building programs especially digitization related in agriculture
- Passionate about climate science, climate adaptation, and climate service provision.
- Basic knowledge of French

**Responsibilities**
- Provide expertise in collecting climate and agricultural systems information and applying climate analytics to understanding temporal and spatial dynamics of climate data.
- Collection of parameterization information on climate, soils, crop and management which underpin crop modelling frameworks and convert these data into useful parameter files.
- Independently apply crop models to developing decision tree approaches used in climate-informed agro-advisories or for the testing of scenarios related to cropping systems management.
- Collate and process weather forecast information and develop a deep understanding of how to apply forecast information in managing agricultural decision making.
- Lead and assist in field data collection, organizing workshops or surveys for understanding the use of ICT in communicating climate information.
- Co-ordination with partners such as the NARES, government agencies and the private sector as required for the project execution.

**General information:**
The duration of contract for the position is three years. This is a nationally recruited position and IITA offers a competitive remuneration package.

**Applications:** Applications including curriculum vitae, copies of certificates, telephone number, email address, and names and addresses of two referees should be sent to the Country Representative, IITA-Tanzania, Plot No. 25, Mwenge – Coca-Cola Road, Mikocheni Industrial Area P.O. Box 34441, Dar es Salaam, Tanzania or by email to IITA-Tanzania@cgiar.org

Applicants are requested to please indicate the reference number for the position as indicated on the heading of the announcement in your application as well as on the subject of your email if sending by email. If sending by post or hand delivery, please indicate the reference number on your application as well as on the left-hand side of your envelope. Please note that any applications without the reference number indicated will be automatically disqualified.

**Closing date:** Two weeks from the date of advertisement appearing in the newspaper.
**Please note that only shortlisted candidates will be contacted.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hili la mikopo Elimu ya Juu linahitaji mjadala

JANA Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Esther Matiko, aliitaka serikali kufanya marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB), kuwa makato ya asilimia 15 ya mkopo yanaumiza wanufaika.

Novemba, 2016, Bunge lilipitisha muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali namba 8 ya mwaka 2016, pamoja na mambo mengine, ikipendekeza kurekebisha Sheria ya Bodi ya Mikopo. Katika mapendekezo hayo serikali ilitaka mnufaika wa mkopo arejeshe kwa makato si chini ya asilimia 15 ya mshahara wake kila mwezi badala ya asilimia nane iliyokuwapo awali.

Mbunge huyo alisema makato hayo ni makubwa na kuwaumiza wanufaika ambao wengi ni watoto wa maskini.

Alikwenda mbali zaidi na kusema Watanzania wengi waliomaliza kidato cha sita wanatamani kupata mikopo ya elimu ya juu, ili kuwa na wataalamu wa fani mbalimbali, lakini mikopo inayotolewa ina makato makubwa na wengi hawaimudu.

Aidha, alitaka kufanyika marekebisho ya sheria hiyo na kurudi kwenye tarakimu moja ya asilimia nane au tano.

Hata hivyo, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, alisema lengo ni kuwezesha mikopo ijiendeshe kwa wanufaika kurejesha mikopo na makusanyo yatosheleze kutoa mikopo kwa wanafunzi wengine.

Waziri huyo alifafanua kuwa makusanyo ya mikopo yanachangia kwa asilimia 46 ya bajeti ya mikopo, asilimia 15 anayokatwa inabaki asilimia 85.

Kilio cha wanufaika wa mikopo hii kimekuwa cha muda mrefu na wengi hasa wa fani za Udaktari wametoa hadi mchanganua inayoonyesha kuwa watakatwa mikopo hiyo na hawatamaliza hadi wanastaafu na pensheni yao itakatwa.

Wengi wanasema tangu kuongezeka kwa makato hayo ambayo yaliwakuta na mikopo mingine ya muda mrefu kiasi cha kupelekea kiasi cha fedha wanachobakiwa nacho kisitosheleze mahitaji na kuishi kwa msongo wa mawazo kiasi cha kushindwa kutekeleza vyema majukumu yao.

Ingawa serikali ina hoja kwamba mikopo hiyo hairejeshwi kwa wakati na lengo la kuweka kiwango hicho ni kutaka kuongeza kiwango kinacholipwa ili kusaidia wakopaji wengine, lakini bado tunaona kuna umuhimu wa kuwa na majadala wa kiwango hiki.

Kwa hali ya sasa ambayo upatikanaji wa ajira bado ni changamoto kubwa mamia ya wanafunzi wanamaliza vyuo vikuu, lakini hawana ajira, jambo ambalo linazua maswali ya namna mikopo hii itakavyorejeshwa.

Kama mtu hana fedha na hana ajira maana yake uwezekano wa kurejesha mkopo ni mdogo, na kwa kadri muda unavyosonga na halipi ndivyo deni linazidi kuongezeka.

Kilio hiki kisipewe kisogo bali kiwafikirie watu wote na ikiwezekana riba inayotozwa na kiwango kiwe inachohimilika kiasi kwamba hadi mtu anastaafu anakuwa amekamilisha kulipa mkopo wake.

Kukiwa na mijadala ya mara kwa mara lazima kutakuwa na maoni ya nini cha kufanya ili kupunguza mzigo mzito kwa mkopaji ambaye baada ya kumaliza masomo anaanza maisha ya familia ambayo inahitaji kuhudumiwa ikiwamo kusomesha watoto, kuhudumia wategemezi na wengine.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Vyakula hivi njia ya kuepusha upatikanaji watoto wa aina hii

**MOJA** ya matatizo ambayo hujitokeza kwenye baadhi ya familia na kusababisha ndoa kusambaratika au wanawake kunyanyapaliwa, ni kupata watoto wenye vichwa vikubwa na wa mgongo wazi.

Ni hali inayotoa msukumo wa kuelimishwa kuhusu chanzo cha tatizo hilo, ambayo wataalamu wanasema inaweza kuepukika, iwapo wahusika watazingatia ulaji wa vyakula vyenye viinilishe vya 'folic acid' vyenye vitamini B9.

Hivyo, kwa kawaida, vina mchanganyiko wa vitamini nyingine tofauti tofauti kama...'folic acid' ni aina ya Vitamini B9 ambayo huchanganyika na maji, muhimu katika utengenezaji dutu za jeni.

Inatajwa katika utengenezaji chembe hai nyekundu za damu, huzuia magonjwa ya uziwi (kupoteza kusikia) na kulinda afya ya ubongo ya mtoto tumboni.

Ili kuipata hivyo, vyakula vya kula ni mboga za majani na matunda vinaepusha uwezekano wa kujifungua mtoto wenye kichwa kikubwa na mgongo wazi, kwa sababu ya kukosekana virutubishi na madini mbalimbali kwa mama.

Hivyo, inashauriwa kinamama walio katika umri wa kupata mtoto watumie vidonge vya 'folic acid' miezi mitatu kabla ya ujauzito, pia bila kukosa mlo wa jamii ya maharage, choroko, bamia na kunde.

Ni bahati mbaya inaelezwa uelewa mdogo na baadhi ya watu kutojali maelekezo hayo, kunakosababisha kuendelea kuzaliwa kwa watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi.

Katibu wa Chama cha Wazazi wa Watoto Wenye Vichwa Vikubwa Mkoa wa Dar ea Salaam (ASBAHT), Milton Byemerwa, anasema msichana anayetarajia kuolewa anatakiwa kuanza kutumia 'folic acid' asisubiri kupata ujauzito.

Kwa maelezo ya katibu huyo, ni vyema wanawake ambao ndio walezi wa watoto wenye matatizo ya vichwa vikubwa na mgongo wazi, wachukue hatua sahihi za kuepuka tatizo hilo, ambalo linawasababishia unyanyapaa.

Imekuwa ikielezwa kuwa miaka ya nyuma jamii ilichukulia kuwa mwanamke mwenye umri mkubwa zaidi ndiye mwenye uwezekano wa kuzaa mtoto mwenye kasoro mbalimbali za kimaumbile.

Hata hivyo, kadri miaka inavyokwenda, wanawake ambao bado ni vijana, wanakumbana na hali hiyo kutokana na mfumo wa ulaji wa vyakula huku wakikwepa vile ambavyo vinaweza kuwapusha kuzaa watoto wa aina hiyo.

Aidha, wataalamu wamegundua kuwa tatizo si wanawake tu wanaokumbana na hali hiyo bali hata wanaume, hali ambayo inawabidi na wao kutumia vyakula vinavyotakiwa kabla ya kuamua kujifungua.

Wanandoa wanaohitaji kupata watoto, wanatakiwa miezi mitatu kabla ya kusaka ujauzito, watumie kwa wingi mboga zinazotakiwa, matunda na vidonge vya folic acid badala ya kukimbilia chips kuku tu.

Waliozoea kukwepa vyakula vinavyoepusha kuzaa watoto wa aina hiyo, ni wakati muafaka wa kujiweka katika mazingira salama zaidi, hasa kwa kutumia vyakula vinavyoshauriwa na wataalamu afya.

Si kwamba wanazuia mtu asile chips kuku au chips mayai, bali wanashauri ujali wa vyakula hivyo upunguzwe na badala yake vyenye folic acid ndivyo vipewe nafasi kubwa zaidi.

Serikali ilishaziagiza halmashauri zote nchini kuhakikisha zinatenga shilingi milioni sita kwa ajili ya kushughulikia matatizo ya watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi.

Katika maadhimisho ya kitaifa ya Siku ya Watoto Wenye Vichwa Vikubwa na Mgongo Wazi Duniani, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa TAMISEMI, Selemani Jafo, anatoa wito kuwa wakati serikali ikichukua hatua hizo, jamii nayo ina sehemu yake ya kufanya, ambayo ni kuzingatia maelekezo ya kitaalamu hasa kwa kubadili mtindo wa ulaji.

Mtindo wa ulaji vyakula, uko ndani ya uwezo wa kila mmoja, ili mradi akizingatia maelekezo ya wataalamu wa afya kwani ni hatua ya kuokoa maisha ya watoto wanaotarajiwa kuzaliwa wasipatwe na maradhi kama hayo ya kujaa maji katika vichwa.

HABARI KITAIFA

# Kampeni kusanya kodi ya ardhi yaingiza bil. 70/-

**Na Munir Shemweta,** DODOMA

KAZI ya kuhamasisha ulipaji kodi ya pango la ardhi na kuwabana wadaiwa sugu inayofanywa na Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, imeanza kuzaa matunda.

Matunda hayo yamepatikana baada ya Naibu Waziri kusimamia na kukusanya Sh. 70,640,189,737 hadi Januari 31, mwaka huu.

Kiasi hicho ni ongezeko la Sh. 4,649,481,460.26 kulinganisha na kiasi kilichokusanywa katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2019/20 ambapo wizara ilikusanya Sh. 65,990,208,276.74.

Naibu Waziri Mabula amekuwa katika ziara mikoa mbalimbali nchini kukutana na watumishi wa sekta ya ardhi kuhamasisha na kuwapa mikakati ya makusanyo ya kodi ya ardhi ikiwamo kuwapelekea ilani za madai wadaiwa sugu na kuwafikisha kwenye Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kwa hatua za kisheria.

Pia katika ziara zake, Dk. Mabula amekuwa akikutana na wadaiwa sugu wa kodi ya ardhi zikiwamo kampuni, taasisi za umma na watu binafsi sambamba na kampuni za urasimishaji ambazo baadhi zimeshindwa kutekeleza kazi kwa wakati.

Mkakati wa Naibu Waziri Mabula unalenga pia kuhamasisha umilikishaji ardhi kwa wananchi na kila alipopita aligawa hati za ardhi ambazo kwa mujibu wake, zinasaidia kuondoa migogoro ya ardhi itokanayo na mipaka na wakati huo huo wananchi kuzitumia hati katika shughuli za maendeleo.

Dk. Mabula tayari amefanya ziara katika mikoa ya Morogoro, Pwani, Mtwara, Lindi, Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Simiyu, Mwanza, Mara na Shinyanga ambako kote aliwabana watendaji wa sekta ya ardhi kuhakikisha wanamsaidia Rais John Magufuli kwa kuongeza kasi ya ufuatiliaji makusanyo ya ardhi aliyoyaeleza kuwa ndiyo yanayosaidia utekelezaji wa miradi ya kimkakati.

"Kuanzia sasa wakuu wa idara za ardhi katika halmashauri tutakuwa tunawapima pia katika makusanyo ya kodi ya pango la ardhi. Atakayeshindwa kusimamia makusanyo basi tutaona kuwa huyo hatoshi katika nafasi yake," alisema Dk. Mabula.

Naibu Waziri alinukuliwa mara kadhaa katika ziara zake akisema kazi bado ni kubwa kuhakikisha wizara inafikia lengo lake la kukusanya Sh. bilioni 200 kufikia Julai, mwaka huu.

Mkuu wa Kitengo cha Kodi Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Denis Masami, alisema jana kuwa jijini Dodoma kuwa mwenendo wa makusanyo ya kodi ya ardhi umezidi kuongezeka kutokana na idadi kubwa ya wamiliki kusambaziwa ilani za madai. Alisema hatua hiyo imesababisha kupatikana kwa Sh. bilioni 70.6 hadi Januari 31.

Kwa mujibu wa Masami, Desemba ndio ilioongozwa kwa makusanyo ya kodi ya pango la ardhi kwa kukusanya Sh. 15,051,465,300 huku Januari zikikusanywa Sh. 8,552,061,548.



Mkuu wa Wilaya ya Liwale, mkoani Lindi, Sarah Chiwamba, akihutubia mkutano wa hadhara wa kuhamasisha wananchi kushiriki kwenye shughuli mbalimbali za maendeleo, wilayani humo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# TASAF yaanza kutembelea wanufaika

**Na Richard Makore, MWANZA**

MFUKO wa Maendeleo ya Jamii Nchini (TASAF), umeanza kutembelea wanufaika wa mfuko huo ikiwamo kuangalia shughuli mbalimbali wanazofanya ili kuendesha familia zao.

Baadhi ya maofisa wa TASAF kupitia viongozi wa mitaa wameanza kuwatembelea wanufaika na kuangalia mafanikio yao baada ya kupatiwa ruzuku.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Mwanza jana, mmoja wa wanufaika wa mradi wa TASAF, Magreth Kaberege ambaye ni mkazi wa Mtaa wa Medical Reseach Kitangiri, alisema alianza kupata ruzuku ya serikali kupitia mfuko huo mwaka 2015.

Alisema alikimbiwa na mume wake mwaka 2014, baada ya maisha yao kuwa magumu na kwamba baada ya TASAF kumpa ruzuku ya Sh. 32,000 zilimsaidia mpaka leo ameweza kujenga nyumba ya vyumba vitatu na kuweka umeme na maji.

Alisema baada ya kupata ruzuku hiyo, alianza biashara ya kupika maandazi na kwamba kuanzia hapo aliweza kuweka akiba na kufanikiwa kutunza watoto watano na kujenga nyumba.

"Baada ya kupata Sh. 32,000 nilianza kuuza maandazi na wakati mwingine hela haikutosha ikabidi nikakope dukani unga wa ngano na mafuta, nikiuza jioni napeleka hela za watu," alisema.

Aliongeza kuwa baaada ya kukimbiwa na mume wake, maisha yalikuwa magumu huku majirani zake wakimpa maneno ya kejeli, lakini anasema kwa sasa anaishi vizuri kupitia mradi wake wa mamalishe.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa kikundi cha Uhuru ambacho kinaundwa na wanawake 24 ambao wanapata ruzuku ya TASAF eneo la Kitangiri jijini Mwanza, Mariam Swahiba, alisema, tangu mwaka 2015 wameanzisha miradi ya ufugaji kuku, kuuza dagaa, mgahawa pamoja na kukopeshana fedha.

Alisema kila mwezi wanakutana na mara mbili ili kukusanya fedha kwa ajili ya kusaidiana na kwamba familia zote 24 zina uhakika wa kupata milo mitatu pamoja na kusomesha watoto wao.

Stela Davidi ambaye ni mnufaika wa ruzuku ya TASAF, alisema fedha hizo zimemsaidia na kufanikiwa kusomesha mtoto wake hadi ngazi ya chuo kikuu.

# Mwenyekiji kijiji ashambuliwa kituo cha polisi

**Na Ambrose Wantaigwa,** TARIME

MWENYEKITI wa Kijiji cha Ng'ereng'ere, Chacha Ghati, anauguza majeraha mabaya katika Hospitali ya Wilaya ya Tarime kwa kile kinachodaiwa alishambuliwa na polisi katika Kituo cha Mpakani Sirari.

Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Msafiri Mtemi, alisema ameagiza kuanzishwa uchunguzi na kuchukuliwa hatua askari waliohusika na tukio hilo.

Pia, alimwagiza Mkuu wa Polisi kusimamia matibabu ya kiongozi huyo.

"Ninaelekea eneo la tukio huko Sirari ili kuwasiliana na wahusika wote wa tukio hilo na lazima uchunguzi ufanyike kubaini ukweli kilichotokea kituoni hapo, ili hatua sahihi zichukuliwe na nimeagiza polisi wahakikishe mwenyekiti apelekwe haraka hospitali," alisema.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, alifika katika kituo hicho Jumanne mchana kuomba sababu za vijana zaidi ya wawili kushikiliwa katika kituo hicho na ndipo askari mmoja ambaye jina lake bado halijafahamika alimshambulia kwa fimbo.

"Nilifika hapo kituoni kutaka kufahamu sababu za baadhi ya vijana wa kijiji changu kushikiliwa zaidi ya wiki moja katika kituo cha polisi, lakini ghafla askari mmoja aliyekuwa zamu alianza kunishambulia na mti hadi nilivyookolewa na wasamaria wema," alibainisha Ghati.

Akizungumza na Nipashe kwa simu, Mkuu wa Polisi Nchini, IGP Simon Sirro, alithibitishia kuwapo kwa tukio hilo na kwamba ametoa maelekezo kwa polisi wa Tarime/Rorya kushughulikia suala hilo na kwamba hatua sahihi zitachukuliwa ili haki itendeke.

"Ni kweli ninazo taarifa hizo na tayari tangu jana Jumanne nimeshatoa maelekezo kwa Jeshi la Polisi mkoa wa kipolisi Tarime/Rorya juu ya namna ya kushughulikia tatizo hilo lililotokea katika kituo hicho," alisema.

# CRDB yajifunga kusaidia makandarasi SGR

**Na Neema Emmanuel,**

MWANZA

BENKI ya CRDB imewahakikishia makandarasi, wafanyabiashara na wadau mbalimbali kuwa iko tayari kuwezesha katika utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kutoka Mwanza mpaka Isaka kupitia fursa za uwezeshaji zinazotolewa na benki hiyo.

Hatua hiyo ni kusaidia utekelezaji wa miradi ya kimkakati inayotekelezwa na serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi nchini.

Hayo yalibainishwa na Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, Abdulmajid Nsekela, wakati wa Kongamano la Mpango Kazi na Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi katika Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) kutoka Mwanza hadi Isaka lililoandaliwa na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), lililofanyika juzi jijini hapa katika ukumbi wa Benki Kuu (BoT).

Alisema CRDB imeweka mikakati mikubwa katika kuhakikisha inaisaidia serikali, makandarasi na wazabuni katika miradi ya kimakakati katika kufanikisha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kwa kufanya uwezeshaji wa moja kwa moja katika miradi.

"Pia tunawawezesha makandarasi na wazabuni kwa maana ya kuwapa mikopo ya utekelezaji wa kazi," alisema Nsekela huku akibainisha kuwa mwaka juzi CRDB ilifanya uwezeshaji wa zaidi ya dola za Kimarekani milioni 40 katika mradi huo.

Kuhusu fursa zinazotolewa na CRDB katika kuwezesha miradi ya kimkakati, Nsekela alisema benki hiyo inatoa huduma ya dhamana kwa makandarasi au wateja ambao wanatafuta kandarasi ijulikanayo kama 'Bid Guarantee' ambayo inawezesha kuwajengea makandarasi uwezo wa kupata kazi.

Pia alisema benki inatoa dhamana za utekelezaji wa miradi (Performance Guarantee) na dhamana za malipo ya awali (Advance Payment Guarantee).

"Pia tunatoa mikopo ya utekelezaji wa kandarasi na zabuni bila dhamana yoyote kupitia huduma zetu ili kusaidia makandarasi na wazabuni kutekeleza miradi kwa weledi, ufanisi na kupata matokeo chanya yenye kuleta maendeleo na kuinua uchumi wa taifa letu," aliongezea Nsekela.

Nsekela alisisitiza kuwa ili makandarasi na wazabuni wafanikishe kazi zao kwa ubora hakuna budi taasisi za fedha kujikita katika kutoa huduma bora na zenye kukidhi mahitaji yao kwa kuwa lengo ni kuleta maendeleo, kutoa elimu na kuwawezesha wote wanaoshiriki katika miradi hii ya maendeleo nchini.

Mwenyekiti wa TPSF, Angelina Ngalula, aliipongeza CRDB kuwa mstari wa mbele kuwezesha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo, huku akiwataka makandarasi kuchangamkia fursa hiyo inayotolewa na CRDB katika kukuza na kuboresha utendaji wa kazi zao.



Mchuuzi wa kofia akisaka wateja katika Barabara ya Ali Hassan Mwinyi, eneo la Oysterbay, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kofia moja inauzwa 5,000/- hadi 15,000/- kulingana na ubora wake. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wafanyakazi walia na malimbikizo mishahara

**Na Maulid Mmbaga**

WAFANYAKAZI wa kampuni ya L&F Fisheries ya jijini Dar es Salaam, wamemlalamikia mwajiri wao waliyemtaja kwa jina la Manfredi Lioto kwa kutowalipa malimbikizo ya mishahara yao kwa miezi mitano sasa.

Mmoja wa wafanyakazi hao, Mkande Ally, jana aliiambia Nipashe kuwa kampuni hiyo inajihusisha na usafirishaji wa mazao ya bahari na siku chache zilizopita ilifungwa kwa sababu mmiliki hakuhusisha leseni.

Alisema takribani wafanyakazi wanane hawajalipwa malimbikizo ya mishahara yao na kila wakienda kudai wamekuwa wakizungushwa.

Alisema wamekuwa wakimtaka mwajiri huyo awalipe na amekuwa akiwaambia waende ofisini, ili awalipe lakini wakifika walinzi wake wanawazuia kuingia ndani kwa madai kuwa wamepewa maagizo wasiruhusu mtu yeyote kuingia ndani.

"Mwajiri wetu amekuwa akituzungusha kwa muda sasa kwani kila tukifika ofisini kwake walinzi wanatuzuia. Kutokana na usumbufu tunaosababishiwa, tulilazimika kupeleka malalamiko yetu serikali ya mtaa ya eneo hilo na mtendaji kata alitoa barua na kumpatia mjumbe wa shina hilo Maulid Omary ili atupelekee kwa mwajiri akimtaka atulipe mishahara yetu, lakini mpaka sasa anatuzungusha," alisema Ally.

Mjumbe wa eneo hilo, Maulid Omary, alisema alipokea barua kutoka ofisi ya kata ikimtaka awapelekee wafanyakazi hao kwa mwajiri wanayemdai na alilitekeleza hilo.

Alisema baada ya kuifikisha barua hiyo ofisini kwa Lioto, Msasani, alikutana naye na kumweleza kwamba siku chache zilizopita aliwaita wafanyakazi hao ili awalipe lakini hawakufika.

Hata hivyo, Lioto ambaye alipoulizwa kuhusu tuhuma hizo, alisema wafanyakazi hao wanaishi ndani ya eneo la kampuni na hakuna siku walikwenda na wakazuiwa kuingia kama wanavyodai.

# Serikali yapongezwa kufufua TAFICO

**Na Mbaraka Kambona**

TAASISI za fedha nchini zimeipongeza serikali kwa uamuzi wa kulifufua Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) na kulipa tena nafasi ya kusimamia mnyororo wa thamani wa samaki, huku zikiahidi kutoa mtaji ili kuliimarisha.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB), Japhet Justine, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari muda mfupi baada ya kumalizika kikao kazi cha kujadili maeneo ya uwekezaji ya TAFICO kilichofanyika juzi jijini Dodoma.

Akizungumza kwa niaba ya viongozi wengine wa taasisi za fedha waliohudhuria kikao hicho, Justine alisema TAFICO ni shirika kubwa linaloshikilia mnyororo mzima wa thamani wa samaki, hivyo kufufuliwa kwake kutawasaidia wavuvi kuwa na masoko ya uhakika.

"Tunaipongeza serikali kwa uamuzi huu mkubwa wa kulifufua shirika hili na sisi tumewahakikishia kushirikiana nao katika kutoa mitaji ambayo itaanzia kwa TAFICO yenyewe na wale wote wanaojihusisha katika mnyororo huu wa thamani wakiwamo wavuvi, wasafirishaji na watengeneza barafu," alisema Justine. Alisema kwa sasa kuna zaidi ya wananchi 200,000 wanaojihusisha na uvuvi na kuongeza kuwa hao wote watafungamanishwa katika mnyororo huo wa thamani.

Justine aliongeza kuwa kufufuliwa kwa shirika hilo kutaongeza fedha za kigeni, uhakika wa masoko makubwa ya kimataifa ambayo yataleta mikataba ya kibiashara itakayowarahisishia wadau walioko katika sekta ya uvuvi kukopeshwa mitaji.

"Tunaamini benki ambazo zilikuwa yanapata shida kupata mikataba ya kuwapatia wafanyabiashara wadogo mitaji, sasa kupitia mikataba ya TAFICO italeta ahueni kubwa na kupunguza madhila yaliyokuwa yanazuia benki kutoa mitaji," alifafanua.

"Sisi kama taasisi za fedha zikiwamo benki, Kituo cha Uwekezaji (TIC) na Mifuko ya Pensheni tumekubaliana tutaweka nguvu kwa pamoja kuhakikisha miradi yote 10 iliyobuniwa na TAFICO inayoangazia kutengeneza mazingira thabiti ya uvuvi inasimama kwa awamu nyingine tena ili tija ya shirika ionekane," alisisitiza.

Naye Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dk. Rashid Tamatamah, alisema uendeshaji wa shirika hilo kwa awamu hii utakuwa wa ubia kati ya serikali na sekta binafsi.

Aliongeza kuwa kwa miaka mingi tangu uhuru haukuwapo uwekezaji katika bahari kuu, huku akisema ni matarajio kuwa uwekezaji ukianza katika uvuvi wa bahari kuu samaki wataongezeka mara tatu zaidi ya wanaopatikana sasa.

Pia Dk. Tamatamah alisema shirika hilo likianza kufanya kazi sekta ya uvuvi itaimarika na litasaidia kuzuia uvuvi haramu na kulinda rasilimali za uvuvi katika bahari kuu.

# Polisi yanasa mtandao wizi wa magari

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Polisi mkoani Dodoma limewakamata madalali wa magari, wauza vipuri chakavu na wachanjaji wa magari ya wizi.

Aidha, jeshi hilo kwa kushirikiana na makamanda wa polisi wa mikoa ya Morogoro, Singida, Iringa na Manyara, limedhibiti mtandao wa wizi wa magari ulioibuka Januari mwaka jana jijini hapa.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi katika kikao kazi cha makamanda hao kilichofanyika jijini hapa, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, alisema watu hao wamekamatwa baada ya msako wa jeshi hilo uliofanyika katika maeneo mbalimbali.

"Tumefanikiwa kuwakamata madalali wa magari ya wizi, wauza vipuri chakavu na wachanjaji wa magari ya wizi," alisema Muroto.

Kuhusu wizi wa magari ambao ulitokea Januari, mwaka jana jijini hapa, Kamanda Muroto alisema kwa kushirikiana na makamanda wenzake wa mikoa hiyo, wamedhibiti mtandao huo kutokana na ulinzi ulioimarisha na jeshi.

Kamanda huyo alisema Januari, mwaka jana, kulizuka wizi wa magari kwenye nyumba za watu ikiwamo wizi wa kutumia silaha ambapo wakazi wengi waliibiwa magari yao.

Muroto alisema kufuatia tukio hilo aliamua kushirikiana na makamanda wenzake wa polisi wa mikoa inayozunguka mkoa wa Dodoma na kwa pamoja wameudhibiti mtandao huo kwa kuwakamata wahusika.

"Magari yaliyokuwa yanaibwa yalikuwa yanapelekwa kwenye mikoa inayotuzunguka ambayo ni Morogoro, Singida, Iringa na Manyara. Kwa kushirikiana na makamanda wenzangu tumewakamata wahalifu hao na kuwachukulia hatua za kisheria ikiwamo ya kufikishwa mahakamani," alisema Muroto.

"Lakini tumefanikiwa kuwakamata madalali wa magari, wauzaji wa vipuri chakavu na wachanjaji wa magari kwani wao ndiyo waliokuwa wananunua magari hayo ya wizi na tumefanikiwa kufungua kesi 11 mahakamani."

Alisema pamoja na wizi huo wa magari pia kulikuwa na uvunjaji wa nyumba za watu, wizi wa pikipiki, usafirishaji wa wahamiaji haramu na uhalifu mwingine. Alisema wahalifu hao walikuwa wanatoka kwenye mikoa hiyo ya jirani na Dodoma.

# TAKUKURU 'yawatemesha' vigogo CCM fedha za mikopo ya vikundi

**Na Jumbe Ismailly, IGUNGA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Igunga, imeanza kuwabana viongozi wanne wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wilayani hapa akiwamo Mwenyekiti wa CCM Wilaya, Regina Thadeo.

Viongozi hao 'wametapishwa' fedha walizochukua kutoka kwenye Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu kinyume cha utaratibu.

Wengine walioanza kurejesha fedha walizokopa kinyume cha utaratibu ni pamoja na Katibu wa CCM Wilaya ya Igunga, Mwanamvua Kilo, Katibu wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM), Esther Malenda na Katibu wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) wa Wilaya ya Igunga, Fransisca Rweyemamu.

Kwa mujibu wa Kaimu Kamanda wa TAKUKURU Wilaya ya Igunga, Baraka Kongoche, viongozi hao wanatuhumiwa kuunda kikundi cha wajasiriamali na kutumia picha za baadhi ya watu bila wao kujua kisha kuchukua mkopo wa Sh. milioni 10 kupitia asilimia 10 ya fedha zinazotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kutoa mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Kongoche aliweka wazi pia kwamba pamoja na viongozi hao kufanikisha dhamira yao ya kuomba na kupewa mkopo huo tangu Machi 24, mwaka jana, cha ajabu na cha kusikitisha wameshindwa kuzirejesha kwa mujibu wa makubaliano.

Kutokana na kushindwa huko, alisema walibanwa na taasisi hiyo na kurejesha Sh. milioni 1.5 kati ya Sh. Milioni 10 walizochukua.

Kongoche alisisitiza kwamba atahakikisha viongozi hao wanarudisha kiasi chote cha fedha walizochukua ili zipelekwe kwa walengwa wenye sifa ya kukopesheka.

Kiongozi huyo alitumia fursa hiyo kuwaonya baadhi ya watumishi wa serikali kuacha mara moja kutumia fedha wanazokusanya kwa kutumia mashine kupitia ushuru wa mazao kuzitoa kinyume cha utaratibu uliowekwa kisheria.

Pamoja na TAKUKURU Wilaya ya Igunga kutoa elimu kwenye maeneo mbalimbali juu ya kuheshimu fedha zinazotolewa na serikali kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa wananchi, bado wako baadhi ya watumishi wamekuwa wagumu kuelewa dhana hiyo na kuonya kwamba watumishi wa aina hiyo hawatabaki salama na ni lazima wachukuliwe hatua kali za kisheria.

Alipotakiwa kuzungumzia suala hilo kwa niaba ya wenzake, Thadeo alikiri kwamba kikundi chao kilichukua Sh. milioni 10 zilizotengwa na Halmashauri kwa ajili ya mikopo ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Hata hivyo, alishindwa kutaja jina la kikundi chao na kudai kuwa yeye hakijui kwa kuwa wao walichomekwa tu na kwamba tayari wameshahojiwa na TAKUKURU juu ya fedha hizo.



Mwanafunzi wa mwaka wa tano wa udaktari katika Chuo Kikuu cha Kumbukumbu cha Hubert Kairuki (HKMU), Mayila Mbuki, akimpima shinikizo la damu, Zubeda Saidi, wakati wa kambi ya siku nne ya kupima afya bure, iliyoandaliwa na Hospitali ya Kairuki Mikocheni, katika kituo kipya cha mabasi ya mikoani Mbezi Luis, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kumuenzi mwasisi wa hospitali hiyo. PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waganga wa tiba asili watakiwa kujisajili

**Na Maulid Mmbaga**

MSAJILI wa Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala, Ruth Suza, amewataka waganga wa tiba asili kujisajili pamoja na dawa zao, ili zithibitishwe kwa ajili ya kuwasaidia Watanzania katika kutibu magonjwa mbalimbali.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini, Dar es Salaam, alisema baraza limekuwa likitoa haki ya kutoa huduma katika jamii na wamekuwa wakiwasajili waganga wa tiba hiyo pamoja, vituo vyoa na maduka.

Suza alisema baraza linafahamu kwamba huduma hizo za asili zimeanza muda mrefu, lakini kuanzia mwaka 2017 waliona umuhimu wa kuanza kusajili dawa za asili hasa kutokana na nchi kuwa na wingi wa miti ya asili inayotumika kama dawa na imekuwa ikisaidia vizazi hadi vizazi katika kutibu magonjwa mbalimbali.

"Kutokana na kwamba kilikuwa kitu kigeni, kwa sasa tumeweka utaratibu maalumu ili kazi hiyo iende vizuri na baraza limesajili dawa za asili 46 ambazo zinasaidia katika magonjwa," alisema.

"Napenda kuwapongeza watoa huduma wetu wamekuwa wasikivu sana na kila mara tulipokuwa tunatoa elimu kuwaelimisha wamekuwa mstari wa mbele kuuliza maswali ili kujua taratibu za usajili zikoje," alisema.

Aliongeza kuwa mpaka sasa kwa yeyote anayependa kusajili dawa yake amekuwa anafuata utaratibu wa baraza na pale anapokwama wamekuwa wakimsaidia hadi kukamilika pia aliwasisitiza waganga kutangaza dawa zao.

Alisema katika baraza wanaye mfamasia anayewasaidia kuzifanyia utafiti dawa na kuzithibitisha ambapo wanaangalia ubora na usalama wa dawa katika matumizi ya binadamu.

Alisema waganga watatakiwa kupeleka mfano wa mimea wanayoitumia katika dawa ili kufanyike uchunguzi itambulike kuwa ipo kwa kiasi gani hapa nchini ili ikiwezekana kuanzishwe kilimo cha miti dawa ili isiwe michache.

"Baraza lina fomu maalumu atakayo patiwa mganga na kwenda nayo kwa mchemia mkuu sambamba na sampuli ya dawa yake na kufanyiwa uchunguzi ili itambulike kuwa ni salama kwa matumizi ya binadamu," alisema.

Alisema kazi hiyo ilifanyika kwa bidhaa za tiba asili 46 na wanafanya hivyo kwa ajili ya kutambua usalama wa dawa hizo

Pia alitoa wito kwa waganga wote ambao hawajasajiliwa kwenda na dawa zao ili zisajiliwe na wao wenyewe wasajiliwe ili kusaidia katika magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza.

HABARI BUNGENI

# Mikopo ya wenye ulemavu yaboreshwa

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, imetekeleza maelekezo ya Bunge kuhusu kupunguza masharti katika utoaji mikopo kwa watu wenye ulemavu, ili kuruhusu mtu mmoja mmoja kupata mkopo.

Waziri wa Ofisi hiyo, Selemani Jafo, alisema jana alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Tunza Malapo.

Mbunge huyo alitaka kujua serikali ina mpango gani wa kutoa mkopo kwa mtu anayemlea mtu mwenye ulemavu ambaye hawezi kufanya kazi yoyote kutokana na ulemavu wake.

Akijibu swali hilo, Waziri Jafo alisema serikali imekuwa ikiboresha mfuko wa utoaji mikopo kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ili kufanya vizuri.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha watu wenye ulemavu wanashiriki vizuri kwenye shughuli za kiuchumi.

"Katika uboreshaji wa kanuni za utoaji mikopo kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kama ambavyo Kamati ya Bunge ya Utawala za Serikali za Mitaa pamoja na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, hivi sasa mtu mwenye ulemavu hata mmoja anapata mkopo na hayo yalikuwa maelekezo ya bunge," alisema.

Alibainisha kuwa mfuko huo awali ulikuwa haufanyi vizuri, lakini kwa taarifa aliyoitoa mwaka jana Sh. bilioni 124 zilitolewa katika vikundi hivyo nchini.

"Kwa taarifa yetu ya miezi sita hadi Desemba, 2020, Sh. bilioni 22.45 zimeelekezwa kwenye makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu," alisema.

Katika swali la Msingi, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Pindi Chana, alihoji serikali ina mpango gani wa kuboresha mikopo ya asilimia 10 kwa ajili ya makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ili kutoa viwango vikubwa zaidi vya mikopo.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa TAMISEMI, Dk. Festo Dugange, alisema mikopo hiyo inatokana na asilimia 10 ya mapato kutokana na vyanzo vya ndani vya halmashauri.

Alisema ili kuboresha kiwango cha mikopo inayotolewa na halmashauri, serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwamo kuzisimamia halmashauri kutekeleza Sheria ya Mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, kuzijengea uwezo kamati za huduma za mikopo za kata na halmashauri ili ziwe na ujuzi wa kutosha wa kuanzisha na kuendeleza vikundi vya wajasiriamali.

# Ukusanyaji madeni benki zilizofutiwa leseni wafanyiwa kazi kupata fedha

BUNGE limeelezwa kuwa ukusanyaji mali na madeni ya benki saba zilizofutiwa leseni na Benki Kuu ya Tanzania unaendelea kufanywa na Bodi ya Bima ya Amana (DIB) ili kupata fedha za kuwalipa wateja wenye amana za zaidi ya Sh. milioni 1.5.

Mwaka 2017 na 2018, BoT ilizifutia leseni ya kufanya biashara ya kibenki Benki ya FBME, Benki ya Wananchi Mbinga, Njombe, Meru, Benki ya Wakulima Kagera, Efatha na Benki ya Wanawake Covenant.

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mwanaidi Ali Khamis, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Jang'ombe (CCM), Ali Hassan King.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji serikali imefikia hatua gani katika kufuatilia fedha za wananchi zilizoko katika benki ambazo zimezuiwa kuendesha shughuli zao hapa nchini.

Naibu Waziri huyo alisema baada ya kuzifutia leseni benki hizo, BoT iliiteua DIB kuwa mfilisi.

"Katika kutimiza wajibu wake wa msingi kisheria, DIB ilianza kazi ya kulipa fidia ya Bima ya Amana ya hadi Sh. milioni 1.5 kwa waliostahili kulipwa bima ya amana katika benki hizo na zoezi (kazi) hilo (hiyo) bado linaendelea (inaendelea) kwa wateja ambao hawajajitokeza kuchukua fidia," alisema.

Aidha, alisema DIB inaendelea na ufilisi wa benki hizo na hadi mwishoni mwa Desemba, mwaka jana Sh. bilioni 4.9 zimeshalipwa kwa wateja wenye amana wa benki sita za wananchi isipokuwa FBME.

Alisema malipo hayo ni sawa na asilimia 77.27 ya Sh. bilioni 6.3 zilizotengwa kwa ajili ya kulipa fidia.

"Aidha, wateja waliolipwa ni 21,675 kati ya wateja 57,076 ikiwa ni asilimia 37.98 ya wateja waliokuwa na amana zilizostahili fidia," alisema.

Kuhusu FBME, Naibu Waziri huyo alisema hadi mwishoni mwa Desemba, mwaka jana, Sh. bilioni 2.4 zililipwa kwa wateja wenye amana ambazo ni sawa na asilimia 52.13 ya Sh. bilioni 4.6 zilizotengwa.

Alisema wateja waliolipwa ni 3,443 kati ya wateja 6,628 ambao ni sawa na asilimia 51.95 ya wateja waliokuwa na amana zilizostahili fidia.

"Wateja waliokuwa na amana inayozidi Sh. milioni 1.5 watalipwa kiasi kilichobakia chini ya ufilisi ambapo kwa mujibu wa sheria na taratibu za ufilisi kiasi kitakacholipwa kitategemea fedha zitakazopatikana kutokana na kuuza mali za benki husika," alisema.

Akiongezea majibu, Waziri wa Katiba na Sheria, Mwigulu Nchemba, alisema utaratibu wa malipo kwa wateja wa FBME umechukua muda mrefu kwa sababu benki hiyo ilikuwa inafanya kazi katika nchi mbili tofauti.

Alisema hali ilisababisha utaratibu wa kukusanya mali na kuzibadilisha kuwa fedha na wateja walipwe uchukue muda mrefu.



Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, akijibu mmoja ya maswali yaliyoulizwa na wabunge kwenye mkutano wa 12 unaoendelea jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**




**Habari na Augusta Njoji**

# Kigoma kuunganishwa umeme gridi ya taifa

SERIKALI imesema ujenzi wa mradi wa kuunganisha umeme Mkoa wa Kigoma katika Gridi ya Taifa, umeanza kutekelezwa Januari, mwaka huu, na unatarajiwa kukamilika Juni, 2022.

Mradi huo unagharimu Dola za Marekani milioni 187 chini ya ufadhili wa Serikali ya Tanzania, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Benki ya Maendeleo ya Korea (EDCF).

Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato, alisema jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Kasulu Vijijini (CCM), Augustine Vuma, aliyetaka kujua ni lini mkoa huo utaunganishwa kwenye gridi ya taifa.

Naibu Waziri alisema mkoa huo unapata umeme kupitia mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia mafuta ya dizeli ambayo ni gharama kubwa kwa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na serikali kwa ujumla.

Alisema katika hatua za haraka serikali inatekeleza mradi wa kuunganisha mkoa wa Kigoma katika gridi ya taifa kutoka Tabora.

"Mradi huo utahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 132 kutoka Tabora hadi Kigoma kupitia Urambo na Nguruka umbali wa kilomita 395 pamoja na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme wa msongo wa kilovoti 132/33 vya Urambo, Nguruka na Kidahwe mkoani Kigoma," alisema.

Alisema gharama za mradi ni Sh. bilioni 142.7 na ujenzi wa mradi ulianza Juni, mwaka jana na unatarajiwa kukamilika Juni, 2022.

Hata hivyo, alisema katika hatua nyingine, serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa njia kuu ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 yenye urefu wa kilomita 280 kutoka Nyakanazi mkoani Kagera hadi Kidahwe mkoani Kigoma.

Alisema mradi huo unahusisha ujenzi wa vituo viwili vya kupoza umeme msongo wa kilovoti 400/220/132/33 na 400/132/33 vya Nyakanazi na Kigoma vyenye transfoma mbili zenye ukubwa wa 120MVA na unagharimu Dola za Marekani milioni 187.

ama
ALHAMISI FEBRUARI 4, 2021
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Wakatili kijinsia, watoto walivyo kaa la moto visiwani Zanzibar**



Ukurasa 14

**Hospitali mpya yaanza kazi kwa upimaji afya bure, foleni siku 3**

# Dk. Gwajima anapoanika silaha ya asili kumkabili mgeni corona

## •Naibu Waziri: Vituo afya, si kila mafua...

**Na Yasmine Protace**

ELIMU inayotolewa na wataalamu wa afya kwa jamii mara zote ndio mkombozi kwa jamii kujikinga na magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza.

Pia jamii ina wajibu wa kuzingatia elimu inayotolewa na wataalamu wa afya, ili kuzidi kujikinga na maambukizi ya magonjwa hayo.

Hivi karibuni serikali imewataka waganga wakuu wa mikoa, wilaya na walio katika vyeo wafawidhi, pia maofisa afya mazingira nchini, waendelee kuimarisha mifumo yote ya udhibiti na kinga ya magonjwa kwa kushirikiana na wananchi, ili kudhibiti magonjwa yote ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, anafafanua kuwa viongozi hao wanatakiwa kuwakumbusha wananchi kwamba elimu ambayo wizara imekuwa ikitoa, ikiwamo ya usafi, kujifukiza, kufanya mazoezi, kula lishe bora na kunywa maji mengi bila ya kusahau matumizi ya tiba asili, ambayo taifa hili limejaaliwa.

"Serikali itaendelea kuchukua tahadhari zote za ufuatiliaji wa mwenendo wa magonjwa yote kama ambavyo imekuwa ikifanya siku zote na kuendelea kuelimisha wananchi juu ya hatua za kuchukua," anasema.





Naibu Waziri, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, DK. Godwin Mollel (kushoto) na kulia kwake ni Waziri mwenye dhamana, Dorothy Gwajima akiisitiza jambo, katika kikao hicho. **PICHA ZOTE: YASMINE PROTACE**

Dk. Gwajima anasema, wizara yake haina mpango wa kupokea chanjo ya Covid -19 inayoripotiwa kuwapo na kutumika kwenye mataifa mengine, serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ina taratibu zake za kufuata inapotokea bidhaa ya afya na kunafanyika baada ya serikali kujiridhisha na sio vinginevyo.

Kwa upande wa Tiba Asili, Dk. Gwajima anasema wizara kwa kushirikiana na Mkemia Mkuu wa Serikali, Baraza la Tiba Asili na wananchi wajuzi wa tiba asili, tayari wameshafanya usajili wa bidhaa (dawa) za tiba asili, alizitaja miongoni mwa dawa hizo;

**MBADALA ULIOPO**

Dk. Gwajima, anaongeza bidhaa za mafuta tete ambayo imehakikiwa na Mkemia Mkuu wa Serikali ni salama na zinatumiwa na watu mbalimbali na zingine zitaendelea kutajwa na Baraza la Tiba Asili.

"Uko ushahidi wa kutosha kabisa kuhusu watu wengi ambao wamepata nafuu na kupona magonjwa mbalimbali ya kuambukiza na yasiyo kuambukiza, yaliyokuwa yanawasumbua baada ya kutumia dawa za tiba asili hata kama walikuwa kwenye matibabu mengine ya dawa za hospitali," anasema.

Waziri huyo anaielekeza Baraza la Tiba Asili/Mbadala kutoa orodha ya dawa zote zilizopitia utaratibu wa kufanya uchunguzi wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali na kuonekana matokeo ya awali ya uchunguzi ni salama kwa matumizi, sasa zinatumiwa na wengi na inawaponya.

Dk. Gwajima anawataka wataalamu na wajuzi wa tiba asili, pia wasisite kujitokeza kufuata taratibu za kuwasilisha dawa na bidhaa zao kwa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, zifanyiwe uchunguzi wa kimaabara, kabla ya kukabidhi taarifa ya matokeo ya uchunguzi kwa Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala.

Pia Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, anakumbusha msisitizo waziri katika kujikinga na serikali imefanya maboresho kwenye viwanja vya ndege, mipakani pamoja na sehemu za kupima magonjwa mbalimbali, ili yasiingie nchini kupitia wageni na wenyeji watokao nje ya mipaka.

"Tiba asili sio jambo la leo, tumezaliwa tumeona kinamama zetu wanatumia baadhi ya majani kwa kutibu mafua au homa na kujifukiza na baada ya hapo, wanatoka salama na kuendelea na kazi. Hivyo tiba asili haijatokana na ugonjwa wa corona bali ni kutoka enzi na enzi".

Dk. Mollel anasema hatua za usafi zinatakiwa kuongezwa nguvu, huku akiwataka wataalamu wa afya kuacha fikiria kila mgonjwa mwenye mafua anayeenda kituo cha afya anaumwa corona, bali majibu yako katika ukweli wa kumpima, ndio wachukue mwelekeo sahihi na tiba yake, kwani kuna wengi wanaoumwa mafua, pasipo corona.

AFYA

# Wakatili kijinsia, watoto walivyo kaa la moto visiwani Zanzibar

- Simulizi ya mtoto inayovuta machozi
- Save Children 'wanunua kesi' kukabili

**Na Getrude Mbaga, aliyekuwa Zanzibar**

LICHA ya kuwapo juhudi za serikali kukomesha ukatili na udhalilishaji kwa watoto, bado pande zote za muungano kunaripotiwa matukio ya ukatili wakikosa msaada wa karibu na haraka, wakati wanapohitaji.

Ripoti zinaonyesha kuwapo udhalilishaji wa watoto ikiwamo ubakaji Zanzibar bado kuna tatizo kubwa lenye athari kwa watoto, hata kufungua utashi wa hitaji serikali kuingilia kati katika kukabili athari hizo.

Takwimu za Jeshi la Polisi ni kwamba kuna jumla ya kesi 1,091 za ukatili na udhalilishaji ziliripotiwa katika vituo mbalimbali Unguja na Pemba mwaka 2017/18 ikilinganisha na kesi 2,449 zilizoripotiwa mwaka 2016/17.

Kuna hatua zinaendelea kuchukuliwa visiwani kuikabili hali hiyo, wakiwamo wadau wa mashirika ya kimataifa ya kutetea haki za watoto la Save The Children kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

Ulinzi wa mtoto, haki za watoto na utawala ambao umenufaisha maelfu ya familia visiwani humo, Juma (sio jina lake halisi) ni mmoja wa vijana visiwani humo walionufaika na mradi huu, kwa kusaidiwa kutoka kwenye mateso ya uanasayansi na udhalilishaji aliyokuwa anafanyiwa na watu wake wa karibu.

"Nimepitia mateso ya udhalishaji na ulawiti wa hali ya juu na hii inaniumiza sana, walikuwa wananifanyia ukatili huo ni watu wangu wa karibu kabisa," anasema Juma, kijana mwenye umri wa miaka 14.

Akizungumza hivi karibuni wakati maofisa wa Shirika la Save The Children walipowatembelea wanufaika wa mradi visiwani humo, Juma anasema maisha yake yalibadilika kuwa machungu, pindi baba na mama yake walipotengana.

"Baada ya wazazi kutengana baba alituchukua kwa nguvu mimi na kaka yangu kwenda kuishi na shangazi yetu, hata yeye alikuwa akiishi hapo. Wakati huo mimi nilikuwa na umri wa miaka sita.

"Maisha yalikuwa magumu sana pale kwa shangazi na wakati mwingine kushinda njaa, bila kula chochote kwa sababu hata shangazi naye hali yake kimaisha ilikuwa duni," anasema.

Anasimulia mkasa wa baba yao aligeuka mlevi kupindukia akijenga mazoea ya kuondoka asubuhi na kurudi usiku wa manane bila kuwaachia chakula na mahitaji ya shule.

Juma anaendelea: "Alikuwa mara zote anagombana na shangazi juu ya tabia yake hiyo, lakini hakubadilika. Baadaye kaka yangu alishindwa na kuamua kutoroka na kurudi nyumbani kwa mama.

"Mimi nilibakia na niliendelea kuvumilia maisha yale magumu, lakini mwishowe niliacha shule na kulazimika kuanza kuzurura mitaani kutafuta chochote chakula, baba yetu alikuwa mkali sana kupitiliza na alinitishia nisije nikaondoka pale nyumbani."

"Nilianza kwenda kushinda maeneo ya fukwe za bahari au kutafuta kusaidia kutafuta samaki na wavuvi ili tu niweze kula na ndipo maisha yangu yalipoharibika kabisa," anaeleza Juma.

Katika simulizi yake anasema, ufukweni walikuwapo vijana wengine wa rika yake na waliomzidi wanaoshinda huko na wanavuta bangi na sigara, hukuiwakianza maozea ya kumuonea na kunidhalilisha.

Juma ana simulizi: "Walikuwa wananipa vilevi kabla ya kunifanyia ukatili huo (ulawiti), iliniuma sana, nililia na kuvumilia, lakini baadaye nikawa sina jinsi ya kufanya.



Aliyekuwa Waziri wa Afya Zanzibar, Mahamoud Thabiti Kombo (kulia), alipokata utepe kuashiria ufunguzi wa Kituo cha Mkono kwa Mkono, kilichoko katika Hospitali ya Micheweni, Pemba, mwaka 2017.

### ARUDI KWA MAMA

"Baada ya miaka kadhaa niliamua kuondoka kurudi kwa mama, nilimweleza maisha ninayoishi na ninayofanyiwa. Mama yangu alipata mshtuko na baadaye alikasirika sana, akanichukua nakwenda kuripoti kesi hiyo Kituo cha Polisi na wale walionifanyia wakatafutwa," anasema.

Juma anasema wakati kesi ikiendelea kwenye vyombo vya sheria ndipo Shirika la Save the Children likamfikia pia ili aweze kupata msaada zaidi wa kisaikolojia na kitabibu.

"Nilianza kupatiwa msaada wa karibu na kituo cha'Mkono kwa Mkono' kilichopo katika Hospitali ya Mnazi Mmoja Visiwani hapa. Nilikutana na madaktari, watu wa ustawi wa jamii, polisi na wengine wengi ambao kwa kiasi kikubwa wamenisaidia kuondoa hasira na chuki iliyokuwa imejaa kwenye moyo wangu.

"Wamenifundisha vitu vingi na mbinu nyingi kuweza kuishi kwa amani na sasa ninaishi vizuri kwa mama yangu. Ananipenda sana na anahangaika kuhakikisha kuwa ninarudi shule," anaongeza Juma.

Kijana huyo anaeleza ndoto yake kubwa ni kuwa mjasiriamali mkubwa kitaifa na ameshaanza juhudi za kuhakikisha kuwa anapata ujuzi wa kumfikisha palipo biashara anayoipenda.

Juma anaiomba serikali na wadau waboreshe zaidi mifumo ya ulinzi wa watoto, ili kuzuia na kushughulikia aina zote za uonevu dhidi ya watoto.

Anataja maeneo hayo ni yanayohusu unyanyasaji wa kijinsia, kutowajali, utandikwaji wa viboko, kufanya kazi hatari, ajira zao katika vikundi vya kivita na ndoa za mapema.

### USTAWI JAMII

Suhaila Abdulla Salim, ni Ofisa Ustawi wa Jamii katika Kituo cha Mkono Kwa Mkono katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja, analalamika tatizo la ukatili na udhalilishaji wa watoto visiwani bado linahitaji juhudi za makusudi kutoka serikalini na wadau wake.

Ofisa huyo, ambaye ni sehemu ya wahusika waliomhudumia Juma katika kituo cha Mkono kwa Mkono, anapatambulisha kuwa:

"Kituo hiki kina timu inayojumuisha maofisa ustawi wa jamii, madaktari na wauguzi, wataalamu wa saikolojia, wanasheria na washauri, hii inatufanya kutoa huduma nzuri pindi tunapopokea mwathirika yeyote wa vitendo vya ukatili." Suhaila anasema, kutokana na darasa la ufanisi la kituo hicho katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja, Asasi ya Save The Children imesaidia uanzishwaji hospitali za Makunduchi na Kivunge, Unguja, pia Chakechake, Micheweni na Wete vilivyoko Pemba.

### CHANGAMOTO ZIKOJE?

Suhaila anasema, katika kupambana na vitendo hivyo vya udhalilishaji watoto, kumekuwapo na hatua mbalimbali zikiwamo za kupata ushirikiano mdogo kutoka kwa jamii.

"Baadhi ya wazazi wamekuwa wakikaa kimya pindi watoto wao wanapotia ukatili wamekuwa wakiamua kumaliza kindugu na kimya kimya, hivyo kuathiri ukuaji watoto hao," anasema.

Dickson Megera, ni Ofisa wa Ulinzi na Utawala wa Haki za Watoto, kutoka Asasi ya Save The Children, anasema vita dhidi ya ukatili kwa wanawake na watoto, inahitaji nguvu za pamoja kutoka serikalini na wadau kwa ujumla.

Megera anasema, mradi huo wa Ulinzi wa Mtoto, Haki za Watoto na Utawala unalenga kuhakikisha jamii yote inapata uelewa wa kina kuhusu ukatili na namna ya kupambana nao.

"Tunataka jamii ijue jinsi ya kugundua viashiria vya ukatili na hivyo kuweza kuepukana nao," anasema na kuongeza: "Hata pindi wanapofanyiwa vitendo vya ukatili, waweze kutoa taarifa kwenye mamlaka husika, ili msaada wa haraka uweze kutolewa ikiwa ni pamoja na kuwachukulia hatua za kisheria wahusika."

Anasema, wamelenga kuwapa uwezo maofisa maendeleo ya jamii wa wilaya, waimarishe madawati yanayotetea haki za watoto, muundo wa uratibu katika ngazi zao na kuzuia ukatili kupitia jumuiya ya wazazi, shule na watoto wenyewe.

### CORONA NA YAKE

Megera anasema katika kipindi cha maradhi ya corona nchini, pia watoto wamefanyiwa udhalilishaji mkubwa hasa wakati walipokuwa nyumbani kwenye likizo ya miezi mitatu, hatua iliyoifanya Save The Children kuingilia kati kutetea haki na ulinzi wa haki za watoto.

"Ni kweli kilikuwa kipindi kigumu kwa watoto, kwani wengi walikuwa nyumbani bila kitu chochote cha kufanya. Kuna baadhi ya wahalifu walitumia mwanya huo wa likizo ndefu kuwalaghai watoto na kuwafanyia utakili ikiwamo kuwalazimisha ngono, kuwalawiti na wengine walipata vipigo, anasimulia mkasa.

Anasema, ni jambo lililowafanya kuchukua hatua ya uelimishaji wa-

Endelea Uk. 13

AFYA

# Sababu zinazomfanya mama asipate ujauzito mwaka mmoja

Na Christina Mwakangale

KATI ya mambo yanayomfanya mwanamke akose ujauzito, inajumuisha maumbile.

Bingwa wa Magonjwa ya Uzazi na Kinamama kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Living Colman, anasema wanandoa au familia wenye lengo kupata mtoto bila ya mafanikio kwa wastani miezi hadi mwaka, inamaanishaa kuna tatizo.

Dk. Colman anasema kutopatikana mimba kuna sababu nyingi za pande zote, mume na mke; mojawapo ni hitilafu kwenye shingo ya kizazi cha mwanamke na wapo ambao kimaumbile, walizaliwa bila ya mirija ya uzazi.

"Baada ya mwanamke kukutana na mwenzake, mbegu lazima zifike katika shingo ya kizazi, ikiwa imeziba au anatoa kemikali nyingi zinazoua mbegu mimba haitapatikana," anasema bingwa huyo.

Pia, anasema mchakato wa kutungwa mimba, huanza kwa mbegu kusafirishwa kutoka mlango wa kizazi kwenda katika mirija, hadi kukutana na yai.

"Kama mirija itakuwa imeziba au mirija haipo, kimaumbile, maana yake mbegu na yai la mama hakuna pa kukutana," anaeleza.

Bingwa huyo anasema mchakato unaofuata mimba ikishatungwa, hukaa kwenye mfuko wa kizazi na kama kizazi hicho kina tatizo la kimaumbile, au uvimbe mimba haitastahimili.

Dk. Colman anarejea takwimu za sasa, kati ya wanawake 100 wapo 10 hadi watano wanaoweza kuwa na tatizo la kushindwa kushika ujazito, kutokana na sababu hizo.



Daktari akitoa huduma kwa mjamzito. **PICHA: MTANDAO**

Anarejea kazini kwake Muhimbili, katika kila wanawake watano wanaofika kwa ajili ya masuala ya uzazi, wawili huwa na shida ya kutoshika mimba.

"Wakifika kliniki tunaangalia historia na maelezo yake kuhusu mzunguko wa hedhi yake, inavyokwenda au aliwahi kupata maambukizi katika kizazi.

Dk. Colman anasema, makundi makubwa ambayo hufanyiwa uchunguzi, ni upande wa mirija na kizazi na mwanamke anayekosa siku zake za mwezi kwa kipindi cha miezi sita au mzunguko kuvurugika kila mwezi huchunguzwa homoni zake.

Bingwa huyo anasema, mirija huanza kuchunguzwa, kama mama anashuhudia uchafu kutoka katika maumbile yake na kujirudia, lengo ni kubaini iwapo mirija imeziba.

"Tiba yake iwapo mirija imeziba, inabidi mama kupandikizwa, ila huwa tunamshauri aje na mwenzake hospitali kwa uchunguzi. Mwanaume tutaangalia mbegu zake," anasema Dk. Colman.

Anasema, asilimia 75 baada ya uchunguzi kwa wanawake, sababu huwa ni katika uzalishaji wa mayai na kupatiwa dawa kusaidia mzunguko wa uzalishaji hedhi, kukaa sawa.

Dk. Colman anasema, uzito mkubwa huangalia katika mambo kama uvutaji sigara na vilevi vinavyokwamisha upatikanaji mimba na kuna matatizo mengine sugu yanayochangia mimba isipatikane.

"Kuona uchafu wa muda mrefu, maambukizi kujirudia kunasababisha mirija kuziba," anasema Dk. Colman, akiongeza hata mama aliyetoa mimba pasipo kufuata utaratibu akitumia mbinu za kienyeji, pia ni chanzo cha kutoshika mimba.

"Sheria za nchi haziruhusu kutoa mimba. Utakuta mtu anatumia mbinu zake, kanywa dawa na kuharibu mimba, asipopata tiba, ushauri wadudu wakifika katika mirija inaweza ikaziba," Dk. Colman anaeleza.

**TIBA IKOJE?**

Dk. Colman, anasema kushindwa kupata ujauzito, kunatibika na inapothibitishwa kitaalamu kuwa mama mhitaji hawezi kushika mimba, anapandikizwa teknolojia iitwayo UVF.

Bingwa huyo anasema, pia mwanaume mwenye mbegu zisizo na nguvu kufika katika mji wa kizazi,

anashauriwa kutolewa mbegu ili zichunguzwe.

"Tunaweza kuchukua mbegu ya baba na kuisogeza karibu na kizazi au mirija ya mwanamke, sababu baba kiasili kutungisha mimba kashindwa," anaeleza Dk. Colman.

**UZAZI MPANGO**

Dk. Colman anasema njia za uzazi ikiwamo za homoni ambazo ni kuchoma sindano, vidonge na kuwaweka kitanzi kinamama zimezoeleka kwa muda mrefu, ingawa anatahadharisha kuwapo matumizi holela.

"P2 (vidonge) hutumika kwa sababu maalum na si kila unapokutana na mtu unameza, unaharibu mfumo wa uzazi," anaeleza.

Ushauri wa Dk. Colman, kujengwa mazoea ya kufanyika uchunguzi wa miili na kubaini tatizo la kiafya, akihitimisha kwa kauli: "Ukiwa na uzito mkubwa sana au mdogo sana hata matatizo haya ya uzazi yatakuwapo."

# Wakatili kijinsia, watoto walivyo kaa la moto visiwani Zanzibar

Inatoka Uk. 11

toto na familia jinsi ya kujikinga na kulinda haki zao.

Kiserikali, Megera anasema wanahimiza wajibu wa kuwapo huduma kila kunakofikika penye watoto, kuhamaisha mwitikio wa kutolewa taarifa, programu za uponyaji, urekebishaji na waathirika kuingizwa upya katika kundi.

Pia ni mkakati unaoangalia namna ya kuwapa mafunzo wataaluma na wadau katika hatua za uzuiaji kama vile polisi, walimu, wafanyakazi wa serikali, walezi, maofisa wa mahakama, wataalamu wa afya na watumishi wa kijamii.

Megera anasema dira ya Save The Children, ni kuhakikisha kila mtoto anapata haki yake ya kuishi, kulindwa, kuendelezwa na kushiriki.

Hivi karibuni, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Khamis Hamza Chilo, alipozuru makao makuu ya Polisi jijini Dodoma, aliagiza udhibiti wa udhalilishaji kijinsia katika jamii, sambamba na utoaji elimu kwa jamii kuhusu uzuiaji wa adha hiyo,

Pia anawataka wananchi kuacha tabia ya kumaliza kesi za udhalilishaji wa kijinsia kinyume na utaratibu, badala yake washirikiane na polisi kuutafuta mkondo wa kisheria.

Takwimu za Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia Watoto (UNICEF), zinadokeza uwiano wa mtoto mmoja kati ya wanne duniani wanapitia ukatili na takriban binti mmoja kati ya watano wameshafanyiwa ukatili, walau mara moja katika maisha yao.

Pia ina dokezo kuwa katika kila baada ya dakika tano inayopita, mtoto mmoja hufariki kutokana na madhara ya ukatili.



Wanafunzi wa shule za msingi na sekondari za Micheweni Pemba, waliohudhuria hafla ya uzinduzi wa Kituo cha Mkono kwa Mkono, katika Hospitali ya Micheweni. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

AFYA

# Hospitali mpya yaanza kazi kwa upimaji afya bure, foleni siku 3

## • Mabingwa waalikwa, mwitikio 'usipime'
## • Walengwa namba moja wajasiriamali



Wananchi wa Kivule, wakiwa katika foleni kuhudhurua afya bure upimaji, katika hospitali mpya ya One Health Polyclinic. **PICHA ZOTE: HALFANI CHUSI.**

**Na Halfani Chusi**

USEMI wa afya ni mtaji, msingi wake kwa namna mbalimbali imekuwa ikishindwa kutafsiriwa na wanajamii walio wengi katika utambuzi wa maana yake.

Sura ya tafsiri ni kwamba, mtu hawezi kuwa na nguvu sahihi kushiriki uzalishaji kama hana afya njema. Na msingi wake ndio kilio cha wazalishaji wengi nchini na hususan wajasiriamali.

Hapo ndipo kilio hicho kinampata mmoja wa wafumbuzi, hospitali mpya iliyopo iitwayo Kivule One Health Polyclinic, wilayani Ilala jijini Dar es Salaam, ambayo imeshaanza kuhamasisha jamii.

Mahali hapo, Kivule ni moja ya maeneo katika Kata ya Kitunda, nje kando ya jiji la Dar es Salaam, kilomita kadhaa kutoka eneo la Ukonga Banana, Kusini mwa jiji la Dar es Salaaam.

Ni sehemu inayojumuisha wanavikundi vya ujasiriamali, wanaopatiwa ushauri wa afya zao, kuhusu magonjwa mbalimbali ambayo yamekuwa wakikutwa, baada ya kupima afya.

**DAKTARI BINGWA**

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani katika hospital hiyo, Amina Mguna, ana ufafanuzi kwamba: "Tumeona tuupe kipaumbele Umoja wa Wanavikundi vya Vikundi vya Ujasiriamali Tanzania kwa kuwa humo kuna vikundi vingi vya wajasiriamali na wajasiriamali walio wengi hawana mishahara," anasema na kuendelea:

"Wanatumia zaidi nguvu kusaka pesa, hivyo kama hawatojitambua kiafya, itakuwa ngumu kwao kuendesha shughuli zao za kijasiriamali. Kama mnavyojua afya ni mtaji, huwezi kuwa na nguvu ya kufanya kazi huku ukiwa unaumwa au una shida kiafya

"Ndio maana tumeona katika kampeni hii ambayo tumejitolea ya kupima afya bure katika hospital yetu hii mpya, kwa watu wa Kivule tukaona tusiwasahau na wajasiriamali ambao afya zao ndio nguzo ya kipato. Kupitia Kauli ya Rais (John ) Magufuli, amekuwa akisistiza watu kupima na kutambua afya

"Sisi katika harakati ya kutambulisha hospitali yetu hii mpya, tumeona tuanze na kutoa huduma hiyo na tunajihusiha na upimaji kisukari, presha, tunapima na kuchunguza saratani ya matiti na katika hilo.

"Pia tumeamua kuchukua baadhi ya wataalam kutoka Hospital ya Ocean Road ( Taasisi ya Saratan Ocean Road) ambao wao ni madaktari bingwa wa mogonjwa mengi, ikiwamo saratani ya matiti, " anaeleza.

**WAALIKWA WAONGEA**

Siku chache zilizopita, Nipashe ilishuhudia namna umma uliojitokeza kupima afya na Mkurugenzi Shirika la Vikundi vya Ujasiriamali Tanzania (SHIVUTA), Andrew Koti, anayeishukuru hospitali hiyo pamoja na uongozi wake kuwakumbuka.



Mkurugenzi wa hospitali ya One Health Polyclinic Kivule, Robert Njee, akiwasilisha jambo kwa wananchi waliofika kupima afya bure.

Ni salamu anazozipeleka mahsusi kwa wanavikundi vya ujasiriamali na wakazi wengine wa Kivule, pia majirani waliopewa fursa kupima afya zao bure, kuwapa ushauri na kujitambua, ili wafanye kazi wakiwa na afya njema

"Sisi wajasiriamali bila ya afya, hatuwezi kufanya kitu chochote. Ukiamka mzima ndio kuingiza kwako pesa, sisi ni tofauti na wenzetu wenye mishahara. Serikalini hata akiumwa atapokea mshahara, ataenda kutibiwa ila wajasiriamali mkiumwa ndio umepoteza siku.

"Kwa hiyo hilo ni jambo la kushukuru, kwa mfano kuna baadhi yetu mmoja amekutwa na dalili ya kisukari ameshauriwa na ushauri ameanza kuufanyia kazi na sasa anaendelea vizuri na shughuli zake za uzalishaji mali zinaendelea kama kawaida.

"Sasa bila hao sukari ingepanda ingekuwaje, ingemlazimu asimamishe shughuli zake akashughulike afya yake, sasa huko ni kupoteza pointi kwa sisi wajasiriamali" anatanka Mkurugenzi, katika neno lake la shukurani.

:"Mwitikio umekuwa mkubwa sana, hata sisi hatukutegemea kama kampeni hii ya upimaji wa afya kwa wakazi wa Kivule," anafafanua, Mkurugenzi Muwezeshaji katika hospital hiyo, Robert Njee.

Anaendelea: "(Kampeni) itaendeshwa kwa muda wa siku tatu, ili kuhakikisha kila mmoja anafikiwa na huduma hii muhimu, maana huu mwitikio kadri siku zinavyozidi kwenda watu wanazidi kuongezeka tu."

Dodosa za Nipashe kupata maoni ya wapimaji, wengi waliunga mkono na kukiro pia ubora wa huduma waiopata, wakifurahia kukutana na madaktari bingwa ambao huenda waangekutana naio kwa gharama kubwa na mazingira magumu.

Pia, ikawa ni fursa mpya kwao kupata, tabia na utamaduni mpya wa kupima afya zao, kujua kinachoendelea huku wakiwa wamebeba ushauri stahiki

Kwa mujibu wa Sera ya Afya nchini, afya ya binadamu inatasiriwa katika ukamilifu wa kutokuwa na maradhi, kimwili, kiakili na kijamii, na kutokuwepo kwa maradhi.

Pia, Sera ya Afya katika mwanzo wake wa miaka ya 1990, ilitoa kipaumbele katika utoaji huduma za kinga, tiba, uhamasishaji na utengemao, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

Sera inayotumika hivi sasa inasisitiza: "Katika utoaji wa huduma hizo, msisitizo umeelekezwa katika utoaji wa chanjo, elimu ya afya na kuruhusu upatikanaji huduma hizo bila malipo."



# Ulinzi mtoto wasisitizwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeitaka jamii katika maeneo mbalimbali kuwa mstari wa mbele kumlinda watoto dhidi ya vitendo vya ukatili, ili kuwasaidia kutimiza ndoto zao kupata elimu.

Hayo yalisemwa jana na Katibu Tawala Msaidizi, Mipango na Uratibu wa Mkoa wa Dodoma, Asanterabi Sang'enoi, katika kikao cha Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi wa Mwanamke na Mtoto ngazi ya Halmashauri ya Wilaya Chamwino, kilichoandaliwa na Shirika lisililo la kiserikali la WomanWake Up (WOWAP).

Sang'enoi alisema serikali itaendelea kutoa msukumo kwa jamii ili kuhakikisha watoto wanapata haki zao za msingi kielimu ambayo itawasaidia kusonga mbele katika maisha.

"Jamii inapaswa kuwa mstari wa mbele kuwalinda watoto wetu kwa sababu watoto ni taifa la kesho na ni viongozi wa baadaye, hivyo wanapaswa kuthaminiwa," alisema Seng'enoi.

Alisema serikali itaendelea kusisitiza dhamira ya kumlinda mtoto. Alisema anadhirisha hilo kwa sera, sheria, mikakati na miongozo mbalimbali iliyowekwa katika kuhakikisha haki za mtoto zinalindwa mahali popote.

Ulinzi wa wanawake na watoto, alisema ni jukumu la jamii nzima kuanzia ngazi ya familia na kuendelea, hivyo kila mmoja ana kila sababu ya kushirikiana na serikali kuilinda jamii hiyo.

"Serikali hushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali katika kutekeleza shughuli za maendeleo na WOWAP ni miongoni mwa mashirika hayo, hivyo ni vyema kila mmoja akatambua hilo kuhakikisha watoto na wanawake wanalindwa dhidi ya ukatili," alisema Sang'enoi.

Alisema kupitia mradi wa kutokomeza ukatili wa kijinsia wa kupunguza ndoa na mimba za utotoni katika wilaya ya Chamwino unaotekelezwa na WOWAP umeonyesha ufanisi katika maeneo ambayo mradi unatekelezwa.

Naye Mchumi kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamiii, Jinsia, Wazee na Watoto, Joel Mangi, alisema ukatili dhidi ya wanawake na watoto unaweza kutokomezwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

Alisema jamii ikiendelea kushirikiana suala la ukatili wa kijinsia litaendelea kutokomezwa kadri siku zinavyokwenda.

Mratibu wa WOWAP, Nasra Suleiman, alisema wamekuwa wakitekeleza mradi wa mimba na ndoa za utotoni tangu mwaka 2016.

# Wabeba wagonjwa begani kisa barabara

**Na Peter Mkwavila, BAHI**

WAKAZI wa Kijiji cha Chifutuka, Bahi mkoani Dodoma, wamesema kutokana na ubovu wa miundombinu ya barabara wanalazimika kubeba wagonjwa kwenye machela na kutembea umbali wa kilometa 11 kwenda kijiji jirani cha Magaga kupata huduma ya usafiri.

Diwani wa Chifutuka, Nollo Mwinje, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari kijijini hapo, kuhusu kero zinazowakabili wakazi wa eneo hilo.

Alisema wagonjwa wanapotakiwa kwenda kupata matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma kutoka kijijini hapo, wanabebwa katika machela kutokana na magari kushindwa kupita katika eneo hilo.

Pia alisema mbali na kuwabeba wagonjwa kwenye machela, pia gharama za maisha zimepanda kutokana na wafanyabiashara kupandisha bei ya bidhaa kutokana na ubovu wa barabara.

"Vitu vimepanda mara mbili zaidi baada ya barabara hii kuharibika, hata gharama kwenye shughuli za kilimo pia ziko juu kwa kuwa wanaolimisha kwa matrekta pia wamepandisha kutokana na gharama za mafuta hali ambayo ni hatari kwa maisha ya mwananchi wa kipato cha chini," alisema Mwinje.

Naye Aghayi Mulila alisema kutokana na ubovu wa barabara, wanaopata shida kubwa ni wajauzito wanaotakiwa kwenda kupata huduma kwenye hospitali ya mkoa kutokana na kutumia fedha nyingi kwa ajili ya usafiri.

Mulila alisema kutokana na kero hiyo, wanaiomba serikali kutatua tatizo la barabara hiyo ili kinamama wakombolewe na adha ya kutozwa kiasi kikubwa cha fedha pindi wanapotakiwa kwenda kupata huduma za kitabibu.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Chifutuka, Julius Chilingo, alisema ubovu wa barabara umesababisha hata wanafunzi wanaosoma shule ya sekondari iliyopo Kijiji cha Magaga kutembea kwa umbali wa kilometa 11 na kuwafanya kutowahi masomo yao kwa wakati.

Chilingo alisema ili kuwahi masomo wanafunzi hao wanalazimika kulipa Sh. 20,000 kwenda na kurudi suala ambalo ni gumu kwa upande wao, hivyo wengi wamejikuta wakikaa nyumbani huku wakikosa haki zao za msingi.

Alisema kutokana na adhaa wanayoipata, wanaiomba serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Bahi, kutenga fedha ili barabara hiyo ipitike muda wote.

"Halmashauri ikitenga kiasi kikubwa tutakuwa wametuondolea tatizo hilo wakazi wa eneo hili pamoja na wengine wanaotumia barabara hiyo ambayo ni kiunganisho kikubwa na vijiji vingine ambavyo wakazi wake ni wakulima, wafanyabiashara na wafugaji," alisema.



Binti Magreta Isikoma (11), akiwaswaga punda kuwarudisha nyumbani wakati akitoka malishoni katika kijiji cha Chifutuka, Wilaya ya Bahi, mkoani Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Upimaji viwanja waibua malalamiko

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

UPIMAJI wa viwanja katika eneo la Michese jijini Dodoma, umezua malalamiko kwa wananchi wanaopimiwa, huku wakihoji asilimia 30 ya maeneo yao wanayokatwa na kampuni ya upimaji ya GEO Plan inakwenda wapi.

Kutokana na hali hiyo, Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, ameitisha mkutano wa hadhara ambao uliwakutanisha wataalamu wa ardhi kutoka Jiji la Dodoma, GEO Plan, Kamati ya Urasimishaji Makazi na wamiliki wa maeneo hayo.

Wakizungumza katika mkutano huo jana, wakazi hao walisema wanashangaa wakati wa upimaji wa viwanja kwa wale wenye viwanja zaidi ya kimoja wamekuwa wakikatwa asilimia 30 ya maeneo yao bila kujua zinakwenda wapi.

Mchungaji Nguvumali alisema wamekuwa wakiuliza maswali kuhusiana na hiyo asilimia 30, lakini hawapati majibu hali ambayo inawapa wakati mgumu.

"Tunashukuru Mkurugenzi umekuja hapa kwetu. Tatizo kubwa kabisa ni hii asilimia 30 tunayokatwa katika viwanja vyetu inaenda wapi? Ukikutwa una viwanja zaidi ya kimoja unakatwa asilimia 30 na ukiwa na viwanja vingi vinapunguzwa unapewa vichache, tunaomba majibu mkurugenzi," alihoji.

Naye Domestress Daud alisema kampuni hiyo ya upimaji imekuwa ikiwakosesha usingizi kwa kuwa haiwashirikishi wananchi wakati wa upimaji kama mkataba wa awali unavyotaka.

"Wakati mwingine unasema afadhari ya CDA kuliko hawa wanaotupimia sasa hivi tunaomba mtusaidie, ardhi kwetu ndiyo kila kitu," alisema.

Barbara Adory alisema wenye mashamba waachiwe wapimiwe halafu ndipo walipe viwanja vyao wenyewe badala ya kukatwa hiyo asilimia 30.

Akitoa ufafanuzi juu ya asilimia 30, Mafuru alisema asilimia hizo ziko kisheria na ni kwa ajili ya wale ambao viwanja vyao vimepitiwa na huduma za jamii kama vile shule, soko, barabara.

"Aliyepitiwa na huduma za kijamii tumpeleke wapi? Atapata hapa hapa kwa hizi asilimia 30. Mtu mwenye viwanja 10 atatupa kadhaa ili na mwenzake apate. Jiji tunataka kila kitu kiende kwa haki na kila mmoja apate kiwanja hapa hapa Michese," alisema Mafuru. Kuhusu kampuni ya GEO Plan, Mafuru alisema kuna mamlaka ambazo zinasimamia kampuni za upimaji, hivyo kama itakutwa na makosa itawajibishwa mara moja.

Hata hivyo aliiagiza kampuni hiyo kubandika ramani katika eneo la wazi ili kila mmoja aone alipopimiwa.

Mkurugenzi wa GEO Plan, Sylvan Magari, alisema kampuni yake imefanya kazi kwa weledi katika eneo hilo na hadi sasa viwanja 6,370 tayari vimeidhinishwa.

HABARI MBEYA

# Kukatika umeme kikwazo kwa viwanda Songwe

**Na Nebart Msokwa,** SONGWE

TATIZO la umeme kukatika mara kwa mara mkoani Songwe, limesababisha baadhi ya viwanda katika Kata ya Nanyala, wilayani Mbozi, kushindwa kufanya kazi ipasavyo hali ambayo inadaiwa kupunguza uzalishaji na kuwakosesha wananchi ajira.

Diwani wa Viti Maalum wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, Mesiah Swela juzi alimweleza Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani kuwa tatizo hilo limeathiri kwa kiwango kikubwa uzalishaji katika viwanda vingi vilivyojengwa katika kata hiyo ya Nanyala.

Alisema Katika Kata ya Nanyala kuna viwanda vingi ikiwamo kiwanda cha malumalu, kiwanda cha chokaa na viwanda vingine vya kusindika mazao ya kahawa na mahindi ambavyo vinakwamishwa na tatizo la kukatika kwa umeme mara kwa mara. "Umeme katika mkoa wetu wa Songwe unakatika kila wakati, hali hii inasababisha viwanda vyetu kushindwa kufanya kazi ipasavyo na hata wananchi ambao kazi zao zinategemea nishati ya umeme nao wanapata shida kutokana na kero hiyo, hivyo tunaomba msaada wako tatizo hili liishe," alisema Mesiah.

Alisema mbali na tatizo la kukatika kwa umeme pia kuna baadhi ya vijiji na vitongoji vya kata ya Nanyala ambavyo havijafikiwa na umeme ambapo alimuomba Waziri huyo kuwasaidia maeneo hayo nayo yafikiwe na nishati hiyo.

Kwa uapande wake Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Jenerali, Nocodemus Mwangela, alikiri kuwapo kwa tatizo la kukatika kwa umeme mara kwa mara ndani ya mkoa huo jambo ambalo alisema ni kero kubwa kwa wananchi.

Alisema Serikali imejitahidi kwa kiwango kubwa kusambaza umeme vijijini lakini wananchi hawapati umeme huo kwa kiwango kizuri kutokana na tatizo hlo la kukatika kwa umeme mara kwa mara.

Akizungumzia suala hilo, Waziri Dk. Kalemani alisema tatizo la kukatika umeme mkoani Songwe linatokana na mkoa huo kutokuwa na kituo cha kupozea umeme wa gridi ya Taifa na badala yake unategemea kupata nishati hiyo kutokea mkoani Mbeya.

"Kama mjuavyo mkoa huu ni mpya ambao umegawanyika kutoka mkoa mama wa Mbeya, wakati tukianza mipango ya kusambaza umeme mpaka vijijini, Songwe ilikuwa sehemu ya mkoa wa Mbeya, hivyo kituo kikubwa cha kupozea umeme tukakijenga mkoani Mbeya, hali hiyo ndiyo chanzo cha tatizo la kukatika umeme mkoani hapa," alisema Dk. Kalemani.

Alisema kwa sasa Mkoa wa Songwe una miundombinu ya umeme yenye urefu wa zaidi ya kilometa 2000 na miundombinu yote hiyo inategemea kupata umeme kutoka kwenye kituo cha kupoozea umeme cha Mwakibete kilichopo Jijini Mbeya.

"Kutokana na urefu wa miundombinu ya umeme mkoani hapa na miundombinu hiyo inategemea umeme kutoka Mbeya, jambo la kukatika umeme mara kwa mara halikwepeki maana ikitokea hitilafu hata ndogo mahali popote kwenye miundombinu hii ni lazima umeme ukatwe ili kuirekebisha," alisema Dk. Kalemani.

Aidha, Waziri Kalemani alisema tayari Serikali imeanza mradi mkubwa wa kujenga njia ya umeme mkubwa kutoka Iringa kupitia Mbeya, Songwe, Rukwa hadi Mpanda ambapo kituo cha kupozea umeme huo kitajengwa mkoani Songwe ili kuondoa tatizo la kukatika kwa umeme.

"Tunao mradi mkubwa wa kuleta umeme wa gridi ya Taifa katika mkoa hii, huu utakuwa ni mradi mkubwa ambao pia utatuunganisha na nchi jirani ya Zambia, katika mradi huo tumepanga pia kujenga kituo cha kupoza umeme mkoani Songwe nadhani hili litakuwa ni suluhisho la umeme kukatika mkoani hapa," alisema Dk. Kalemani.




Mhifadhi Mkuu Msaidizi wa Shamba la Miti la Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) Kiwira, Grace Wille (kulia), akikabidhi msaada wa madawati 20 kwa Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Castory Makeula, yaliyotolewa na shamba hilo, kwa ajili ya kusaidia Shule ya Msingi Isyonje, mkoani Mbeya juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**.

## 'Kutokujua sheria kikwazo kupata haki'

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

IMEELEZWA kuwa baadhi ya wananchi wasiojua sheria wanashindwa kupata haki kwenye Mahakama ya Mwanzo kutokana na sheria kutoruhusu ngazi hiyo ya mahakama kutumia mawakili.

Kutokana na hali hiyo, Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) Kanda ya Mbeya, kimeiomba serikali kupitia Bunge kurekebisha sheria ya mahakama hiyo, ili mawakili watumike kuwatetea wananchi wanaohitaji huduma hiyo.

Chama hicho kilitoa ombi hilo wakati wa kilele cha maadhimisho ya wiki ya sheria ambayo yalifanyika kwa wanasheria hao kutoa msaada wa sheria kwa wananchi katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Mbeya na kuhitimishwa katika Mahakama Kuu Kanda.

Mwenyekiti wa TLS Kanda ya Mbeya, Tasco Luambano, alisema sheria ya mahakama Sura ya 11 inawanyima wananchi haki yao ya msingi ya kuwa na mawakili hali ambayo inasababisha washindwe kupata haki yao.

"Hii Sheria sio kwamba inawanyima tu wananchi haki ya kuwakilishwa mahakamani bali inawanyima fursa hata mawakili kufanya kazi ya kuwawakilisha wananchi ambayo ndiyo waliyoisomea," alisema Luambano.

Wakili wa Serikali, Francis Rodgers, aliiomba Serikali kutumia wataalamu wake kubadili Sheria za Mila na kuziingiza kwenye mfumo wa kimahakama ili zisaidie wananchi kupata haki kwenye mhimili huo wa utoaji haki.

Alisema sheria hizo zikiboreshwa zitasaidia kuboresha hata utoaji wa haki kwa maelezo kuwa mfumo wa mahakama ni wa kisasa kuliko ule wa kimila.

Hata hivyo, baadhi ya wadau waliiomba Mahakama kujenga mifumo imara ya utoaji haki ambayo itasaidia wananchi kupata haki hata baada ya miaka 100 ya ijayo.

# TFS yatoa madawati 20 shule ya msingi

**Na Nebart Msokwa, RUNGWE**

WAKALA wa Huduma za Misitu nchini (TFS), kupitia Shamba la Miti la Kiwila lililoko katika Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, umetoa msaada wa madawati 20 kwenye Shule ya Msingi Isyonje wilayani humo, ili kupunguza tatizo la upungufu wa samani shuleni hapo.

Uongozi wa shamba hilo ulikabidhi msaada wa madawati hayo kwa viongozi wa Kijiji cha Isyonje, ambacho ni miongoni mwa vijiji vinavyolizunguka shamba hilo huku ikidaiwa kuwa ni miongoni mwa taratibu za TFS kuimarisha ujirani mwema.

Mhifadhi Mkuu Msaidizi wa Shamba la Kiwira, Grace Wille, alisema waliamua kutoa msaada huo baada ya kuombwa na uongozi wa kijiji cha Isyonje kuwa shule hiyo ina uhaba unaosababisha wanafunzi kukaa watano kwenye dawati moja.

Alisema walipofanya ziara ya kutembelea shule hiyo walibaini kuwa ni kweli shule hiyo ina tatizo la uhaba wa madawati na ndipo wakaamua kutoa mchango huo.

"Huu ni utaratibu wetu kila mwaka kusaidia vijiji vinavyolizunguka shamba letu, mwaka jana tulisaidia ujenzi wa Zahanati katika Kijiji cha Igoma kwa kuchangia mbao na saruju na tutaendelea kufanya hivyo kulingana na mahitaji," alisema Wille.

Alisema kwa sasa wanapata ushirikiano mkubwa kutoka kwa wananchi kwenye utunzaji wa misitu kutokana na wananchi wengi kutambua umuhimu wa misitu hiyo na kwamba moja kati ya vitu vilivyowaangusha wananchi hao ni msaada ambao wamekuwa wakiupata.

Akipokea msaada wa madawati hayo, Mwenyekiti wa Kijiji cha Isyonje, Naomi Mwakuka, alisema madawati hayo yatasaidia kupunguza tatizo kwenye shule hiyo.

Alisema mara nyingi wanafunzi huwa wanashindwa kusoma kwa raha kutokana na kukaa kwa msongamano kwenye madawati na kwamba madawati hayo yatasaidia wanafunzi kusoma kwa raha na kuinua kiwango cha elimu.

Aidha, alisema wamekuwa wakiwashirikisha wadau wengi kwenye uboreshaji wa elimu na huduma zingine za jamii katika kijiji hicho lakini TFS wamekuwa wakiitikia kwa haraka zaidi.

"Nina uhakika hapa hata kiwango cha ufauru wa wanafunzi wetu kitaongezeka, kwenye shule zingine hasa za watu binafsi unatuka kila mwanafunzi anakaa kwenye dawati lake lakini kwenye hizi shule zetu hali ni tofauti," alisema Mwakuka.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Isyonje, Grace Mganga, alisema baada ya kupata msaada huo kuna baadhi ya madarasa wanafunzi watakuwa wanakaa wawili ama watatu tofauti na ilivyokuwa awali ambapo walikuwa wanasongamana zaidi.

Alisema mbali na kupunguza tatizo la upungufu wa madawati lakini aina ya madawati waliyopatiwa yana ubora ambao unawavutia wanafunzi kukaa darasani na kusoma kwa raha na kwamba yatapunguza hata utoro.

Diwani wa Kata ya Isongole kilipo Kijiji cha Isyonje, Mwaningo Sote, aliwaomba wananchi wa Kata hiyo kuendelea kutunza misitu ili waendelee kunufaika na misaada itokanayo na mavuno ya misitu hiyo.

Aliwashukuru TFS kwa msaada huo na kwamba ni chachu kwa wananchi kutunza mazingira kwa maelezo kuwa misitu inasaidia kuleta mvua na kuboresha mazingira.



# Mkataba ujenzi bandari watiwa saini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imetiliana saini na kampuni ya kimataifa ya TANGEN Group juu ya upembuzi yakinifu ujenzi wa Bandari ya Mpiga Duri huko Maruhubi Unguja.

Kazi hiyo itahusisha pia ujenzi wa gati tano pamoja na kiwanda cha kutengeneza vifaa vya uvuvi wa baharini na chelezo cha kutengeneza boti.

Utiaji saini wa makubaliano ya miradi hiyo uliofanyika jana, ulishuhudiwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, Ikulu Zanzibar.

Baada ya utiaji saini huo, Rais Mwinyi alisema huo ni mwanzo mzuri wa utekelezaji wa miradi hiyo ambayo kuzishirikisha sekta binafsi katika ujenzi wa maendeleo na ukuaji wa uchumi.

Alisema miradi ya miundombinu ya kibiashara katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itasimamiwa na kutekelezwa katika mfumo wa ubia.

Serikali, alisema imejipanga kuhakikisha inaleta mageuzi makubwa ya kiuchumi katika uchumi wa buluu ambao kupitia makubaliano yaliyofikiwa, wavuvi wadogo watafaidika kwa kujengewa soko kubwa la kuendesha biashara ya samaki kwa njia ya mnada.

Katika mradi wa ujenzi wa Bandari ya Mpiga Duri katika eneo la ukanda wa Maruhubi hadi eneo la hoteli ya Bwawani, alisema utahusisha ujenzi wa kiwanda cha boti, kiwanda cha kutengeneza nyavu na kusindika minofu ya samaki na mbolea inayotokana na malighafi ya bidhaa hiyo.

Aidha, alisema katika kupunguza safari ya kupeleka vyombo vya baharini matengenezo chelezoni Mombasa nchini Kenya, katika mradi huo mkubwa utakuwa na huduma za matengenezo ya vyombo vya aina mbalimbali.

"Huu ni mradi mkubwa ambao sasa unafunguwa njia ya safari ya Zanzibar kuelekea katika uchumi tuutakao wa buluu, ni fursa kwa sekta mbalimbali ikiwamo wavuvi kujipanga na kuona wanafaidika na miradi hiyo ambao wao ndio walengwa wakuu," alisema.

Kuhusu mradi wa ufufuaji nishati ya umeme ambao umetiwa saini na Mwakilishi wa kampuni hiyo na kwa upande wa Zanzibar kutiwa saini na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Miraji Mgereza Mzee, Dk. Mwinyi alisema utakuwa mkombozi katika kulipatia ufumbuzi tatizo la uhaba wa nishati ya umeme.

Alisema wakati Zanzibar ikielekea katika uchumi wa buluu ambao unakwenda sambamba na ujenzi wa viwanda, suala la upatikanaji wa umeme wa uhakika ni muhimu sana.

Rais Mwinyi alisema kwa sasa mahitaji ya nishati ya umeme kwa Zanzibar hayatoshelezi mahitaji ya safari ya kuelekea katika uchumi wa viwanda kwa kuwa mahitaji kwa Zanzibar ni megawati 100 wakati kwa upande wa Pemba ni megawati 20.

Mwakilishi wa kampuni ya TANGEN GROUP, Allan Kessler, alisema utekelezaji wa mradi huo ni wa kwanza katika bara la Afrika ambao utazalisha ajira kuanzia 3,000 hadi 5,000 katika maeneo mbalimbali.

Alisema mradi huo utaifanya Zanzibar kujitosheleza na kuingia katika uchumi wa buluu kwa mafanikio makubwa kwa sababu huduma zote zinazohitajika ikiwamo matengenezo ya boti za kuvua samaki na vifaa vya uvuvi wa samaki ikiwamo nyavu zinapatikana nchini.

Mradi huo unatarajiwa kugharimu dola za Kimarekani bilioni 6.3 ambao utahusisha pia ujenzi wa bandari mbili za Pemba ikiwamo Mkoani na kuifanya kuwa kiungo kikuu cha lango la Afrika Mashariki.

Katibu Mkuu Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Aboud Suleiman Jumbe, alisema kuwapo kwa mradi wa uzalishaji wa vifaa vya uvuvi Zanzibar ni hatua kubwa ambayo itawawezesha wavuvi kupiga hatua kubwa ya maendeleo





Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk.Hussein Ali Mwinyi akizungumza wakati wa hafla ya utiaji wa saini ya makubaliano ya Mpango Mkuu wa Upembuzi yakinifu juu ya ujenzi wa Bandari Shirikishi ya Uvuvi katika eneo la Mpiga Duri na mkoani Pemba na Mradi wa Ufuaji wa Umeme wa Nishati ya Gesi Zanzibar, Ikulu jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU.**

## Kamati yataka fedha mfuko jimbo kuhojiwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMATI ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi ya kuchunguza mashirika na Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imewataka wananchi kuhoji matumizi ya fedha za mfuko wa jimbo ili kujua matumizi yake.

Hayo yalisemwa jana na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Juma Ali Khatib, alipozungumza na wananchi wa kisiwa cha Kojani Pemba katika ziara ya kukagua miradi ya wananchi ikiwamo ya majisafi na salama.

Alisema fedha za mfuko wa jimbo zinatolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, lengo lake zitumike kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika jimbo.

"Wananchi katika majimbo ya uchaguzi wanatakiwa kufahamu matumizi ya fedha za mfuko wa jimbo ambazo zinatolewa kwa ajili ya shughuli za miradi ya maendeleo. Msiogope kuuliza matumizi ya fedha za mfuko wa jimbo zinavyotumika," alisema.

Pia Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Kuchunguza Hesabu za Wizara ya SMZ ilipata nafasi ya kutembelea majimbo ya Ole, Wingwi, Wawi na Mtambwe na kuona matumizi ya fedha za mfuko wa jimbo zilivyotumika.

Akizungumza katika Jimbo la Ole, aliyekuwa Mwakilishi wa Jimbo hilo, Mussa Ali Mussa, alisema katika kipindi chake cha uongozi miaka mitano, fedha za mfuko wa jimbo zilitumika vizuri katika miradi ya ujenzi wa shule, majisafi na salama na uimarishaji wa vituo vya afya.

Aliipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais katika uratibu mzuri wa utoaji wa fedha za mfuko wa jimbo pamoja na matumizi yake ambayo yamelenga kuleta maendeleo.

# Watakiwa kujenga utamaduni kuchangia damu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANANCHI mkoa wa Kusini Unguja wametakiwa kuwa na utaratibu wa kuchangia damu kwa hiari ili kuokoa maisha ya wagonjwa wenye mahitaji ya huduma hiyo.

Akizungumza jana katika sherehe za shamrashamra ya miaka 44 ya kuzaliwa kwa Chama Cha Mapinduzi (CCM) zilizoandaliwa na Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Mkoa wa Kusini Unguja katika kiwanja cha mpira wa mikono Dunga, Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Rahma Kassim Ali, alisema mahitaji ya damu salama yamekuwa makubwa hasa kwa kinamama wanaojifungua.

Alisema kama zilivyo nchi zingine duniani, Zanzibar nayo ina mahitaji makubwa ya damu salama hasa kwa watoto wadogo, wazazi, waathirika wa ajali na wagonjwa wa upasuaji, hivyo uwapo wa damu nyingi katika hospitali utasaidia kuokoa maisha ya makundi hayo.

Pia alisema kwa mujibu wa takwimu kutoka Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto zinaonyesha zaidi ya chupa 1,350 za damu zinahitajika kwa mwezi, hivyo kila mwenye uwezo wa kuchangia ana wajibu wa kufanya hivyo ili kuona jamii inaondokana na tatizo hilo.

Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Kusini Unguja, Shemsa Abdalla Ali, alisema lengo la UWT mkoani humo ni kuhakikisha wanakusanya zaidi ya chupa mia moja za damu ili kusaidia upatikanaji wa damu salama ikizingatiwa wanawake ndio wenye mahitaji zaidi.

Naye Katibu wa UWT Mkoa wa Kusini Unguja, Asha Khamis Omar, alisema UWT imefikia uamuzi wa uchangiaji damu baada ya kutafakari kuwa siku zijazo kutakuwa na mwezi mtukufu wa Ramadhani, hivyo itakuwa vigumu kupata watu wa kuchangia damu.

Katika uchangiaji damu kwa hiari, jumla ya chupa 224 za damu zimekusanywa na zinalenga kusaidia wagonjwa wenye mahitaji ya damu hizo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**Uza,**
**Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie 0782253676**

## KUPOTEA KWA CHETI



**EDWARD FRANCIS DANIEL** amepotelewa na cheti cha elimu ya kidato cha sita alichomaliza katika Shule ya Sekondari ILULA mwaka 2016 chenye Index: **P0515/0510.** Kwa yeyote atakayekiona anaomba atoe taarifa kituo chochote cha polisi.Taarifa ya polisi: **MAN/BAB/RB/44606/2021.**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**MBUKE MARCO NZELLA** anatangaza kupotelewa na cheti cha ualimu daraja la iii A. kilichotolewa na baraza la mitihani **NACTE** mwaka 2015 kupitia chuo cha **NG'WANZA TEACHERS COLLEGE.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi. **MBE/MBE/RB/64602/2021.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AUGUSTINO A MSIGWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **SCANIA** yenye namba za usajili **T 749 CNW, CHASSIS NO. 01206236, ENGINE NO. 5345711,** yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **MKB/RB/TR/22/2021**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika Mahakama ya mwanzo**
**Mjini Morogoro**

**Usimamizi wa mirathi 25/2021**

**Ombi la GABRIEL ANTONY NYAGALI kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu SIJALI OMARI,**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 4/2/ 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo . Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 22/01/2021

Tarehe 22/01/2021
Sahihi ya Hakimu
Mahakama ya Mwanzo Mjini
HAKIMU
YA MWANZO MJINI
MOROGORO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**
**MAOMBI MADOGO NA. 202 YA 2020**
**BAINA YA**
**PATRICK MSHANA.....................MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**BAHATI GRAMSENI NYAMWESA NA WENZAKE.........WADAIWA**

**KWA: BAHATI GRAMSENI NYAMWESA**
**PAMELA MKONO**
**GILLIFFITHS ELIUSOO LEMA**

**POPOTE WALIPO.**
**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 4.02.2021 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.
**ANAGALIZO: -** kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likidhibitisha kuwa umepokea hayi ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 22 ya mwezi wa Januari,2021.

**ROYAL RUNNER'S AND GENERAL SUPPIES T.LTD &COURT BROKER**

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

TUTAFANYA MNADA TAREHE 04/03/2021 SAA NNE ASUBUHI TUTAUZA KIWANJA PLOT NO.42 BLOCK F CHIDACHI NORTH MALI YA BENEDICT SOSTENES MWILIKO BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MKOPO ALIOKOPA IMARISHA MAISHA LTD, S.L.P.4169 DODOMA. HIVYO TUNAPENDA KUWAKARIBISHA WAHITAJI WOTE.

**KWA MAWASILIANAO PIGA NO. 0713913150/ 0688729841.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**VICTORIA EMMANUEL MUNISI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 224 DRC SUZUKI CARRY.** Chassis No. **DD51T430448.** Engine No. **F6A6384557.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DSM/PHQ/RB/57296/2021.**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika Mahakama ya mwanzo
Mjini Morogoro
Usimamizi wa mirathi 34/2021

Ombi la **LILLY PAULO MOSHI** kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **PAULO PETRO MOSHI,**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe **4/3/ 2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo .
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.
**Tarehe 03/02/2021**

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako la
Nipashe kila siku

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Ajali yaua 32 ikihusisha magari matano

**Kasese, UGANDA**

WATU 32 wamethibitishwa kufariki dunia, kwenye ajali ya gari nchini Uganda, iliyotokea jana usiku katika wilaya ya Kasese.

Vifo hivyo vilitokea baada ya magari matano kugongana katika kijiji cha Kihongo, kilichopo barabara kuu ya Hima -Rugendabara, wilayani humo, Magharibi mwa Uganda.

Miili ya marehemu ilipatikana na huku majeruhi watano wakipelekwa katika Hospitali ya Kilembe.

Taarifa iliyotolewa na Shirika la Msalaba Mwekundu Uganda, timu yao ikishirikiana na Jeshi la UPDF na Polisi iliyoongozwa na Meja Charles Nzei, waliwaokoa majeruhi na kupata miili 32.

Sababu ya ajali hiyo ilitajwa kuwa ni ufinyu wa barabara inayotengenezwa, giza kubwa na kusababisha malori mawili kugongana na kuanguka, mjini Kasese.

Baada ya kuanguka kwa malori hayo, gari lingine kutoka Budibugyo pia lilianguka kwenye katika eneo hilo hilo.

Kwa pamoja magari 5 yalianguka kwenye ajali hiyo, ambayo ilisababisha vifo vya watu 32 na watano kujeruhiwa vibaya, saa 3 usiku, kwa mujibu wa msemaji wa Red Cross, Irene Nakasita.

Kati ya magari hayo, lori dogo ya aina ya kenta lilikuwa limebeba jeneza na watu waliokuwa wakienda kuzika wakitoka wilayani Budibugyo, kwenda Kata ya Maliba.

Kwa mujibu wa takwimu za Jeshi la Polisi nchini Uganda, ajali za barabarani 20,000 hutokea kila mwaka, na kusababisha vifo vya watu 2,000.

Uganda ni miongoni mwa mataifa yenye kiwango cha juu cha ajali za barabarani.

***BBC***




Walinzi wakiimarisha ulinzi mbele ya mlango wa kuingilia kituo cha utafiti cha 'Wuhan Institute of Virology' wakati wa ziara ya timu ya Shirika la Afya Duniani (WHO), Mkoa wa Hubei nchini China, jana, kuchunguza kiini cha chanzo virusi vya corona. **PICHA/AP**

# Wanasheria kukata rufani hukumu ya Navalny

**Moscow, URUSI**

WANASHERIA wa kiongozi wa upinzani Urusi, Alexei Navalny, wamesema watakata rufani kupinga adhabu ya kifungo cha miaka mitatu na nusu jela, alichohukumiwa mteja wao.

Mahakama ilisema, Navalny alivunja sheria kwa sababu hakuwa akiripoti katika mamlaka ya magereza kama ilivyotakiwa, wakati alipokuwa Ujerumani kwa matibabu baada ya kupewa sumu.

Tangu mwaka 2014, Navalny alikuwa akikabiliwa na kesi ya madai ya udanganyifu iliyokuwa imesimamishwa kwa muda.

Kulingana na mawakili wake, huenda Navalny akatumikia kifungo cha miaka miwili na miezi minane kwa vile alishawahi kutumikia kifungo cha nyumbani siku za nyuma.

Olga Mikhailova, ni mmoja wa mawakili wake.

Kabla ya kutolewa hukumu hiyo na mahakama, Navalny alijitetea kwamba asingeweza kuripoti katika mamlaka ya magereza kama alivyotakiwa kisheria, alipoteza fahamu wakati akipelekwa Ujerumani kwa matibabu.

"Nilikuwa nikipatiwa matibabu Ujerumani," alisema Navalny alipojitetea akiwa mahakamani.

Aidha, Jaji alisisitiza kwamba alilazimika kutimiza masharti hayo katika hali yoyote ile.

"Mahakama imeamua kuunga mkono hoja ya Mamlaka ya Wafungwa," alisema Jaji Natalya Repnikova, wakati akitangaza uamuzi wa mahakama.

Navalny alirudia kusema kwamba alipewa sumu kwa amri ya Rais Putin.

Kwa mara nyingine mkosoaji huyo wa Rais Vladimir Putin alizishutumu mamlaka za Urusi kwa kujaribu kumuua kwa kumlisha sumu ya Novichok, inayoathiri neva.

Navalny alirudi Urusi kutoka Ujerumani mapema mwezi huu, licha ya kuonywa kwamba atakamatwa baada ya kuwasili nchini humo.

Tangu alipokamatwa, Urusi imeshuhudia maandamano makubwa ya watu wengi katika wikiendi mbili mfululizo na watu kadhaa kukamatwa na polisi.

Serikali ya Urusi sasa inataka kutuma wanajeshi kulinda shule zote ili kuhakikisha wanafunzi hawashiriki katika maandamano kumuunga mkono Navalny.

Mamlaka za Urusi zimekuwa zikijaribu kuzima maandamano hayo kwa njia yoyote iwezekanayo, ndiyo maana zimelenga shule kwa kuwa waandamanaji wengi ni vijana wadogo.

Kulingana na wanaharakati wa kutetea haki za binadamu, vijana wa chini ya miaka 18 wapatao 205, walikamatwa katika maandamano ya wiki iliyopita, huku maandamano zaidi yakitarajiwa kufanywa baada ya hukumu ya mahakama dhidi ya Navalny.

***DW***

# Aung San Suu Kyi kushtakiwa na utawala wa kijeshi

**Naypyidaw, MYANMAR**

VIONGOZI wa kijeshi waliochukuwa madaraka kwa nguvu nchini Myanmar wanapanga kumfungulia mashtaka ya uhaini kiongozi wa kiraia, Aung San Suu Kyi.

Ripoti zilizochapishwa katika mitandao mbalimbali ya kijamii zilisema uongozi mpya wa kijeshi uliochukua madaraka Kyi, na viongozi wenzake wengine, unapanga kumshtaki mwanasiasa huyo kwa kosa la uhaini.

Kyi alikamatwa katika mji wa Naypyidaw pamoja na Rais Win Myint na maofisa wengine wa serikali katika msako uliofanyika Jumatatu alfajiri.

Jeshi lilitangza hali ya hatari na kumkabidhi madaraka Mkuu wa Majeshi, Min Aung Hlaing, na kisha kutangaza baraza jipya la mawaziri linalojumuisha majenerali, viongozi wa zamani wa kijeshi na wanasiasa kutoka chama kinachoungwa mkono na jeshi.

Ripoti zinaeleza kwamba KyI na wanasiasa wa chama chake cha NLD na wabunge watafunguliwa mashtaka.

Nchini Myanmar kesi ya uhaini adhabu yake inabeba kifungo cha hadi miaka 20 jela na wakati mwingine adhabu ya kifo hutolewa kwa mujibu wa gazeti moja linaloegemea upande wa serikali katika ripoti yake ya mwaka 2018.

***DW***

# Watoto wa5 wauawa shambulio Marekani

**Oklahoma, MAREKANI**

WATU sita, ikiwamo watoto watano, wamefariki dunia katika shambulizi la kutumia silaha.

Tukio hilo lilitokea katika nyumba moja mji wa Muskogee, Jimbo la Oklahoma la Marekani.

Kulingana na taarifa iliyotolewa na Polisi, timu yao ilifika eneo la tukio baada ya kusikia milio ya risasi maeneo ya jirani.

Polisi walimkamata mshukiwa aliyekuwa akitoroka.

Aidha, ilielezwa kuwa watu watano, wanne kati yao wakiwa ni watoto, walikutwa wamefariki ndani ya nyumba hiyo.

Mtoto mmoja na mwanamke walipelekwa hospitalini wakiwa na majeraha, licha ya mtoto huyo kufariki hospitalini na mwanamke huyo kuwa katika hali mbaya.

Polisi hawajazungumza lolote kuhusu mhusika na shambulizi hilo la kinyama, huku uchunguzi ukiendelea.

***TRT***




# UNITED YAREJESHA MATUMAINI EPL

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER United imerudi katika mbio za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu England baada ya kupata ushindi mnono wa mabao 9-0 dhidi ya Southampton katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Old Trafford juzi usiku.

Kwa matokeo hayo, United inarejea katika nafasi ya pili ikiwa imecheza mechi 22 baada ya kufikisha pointi 40, sawa na vinara, Manchester City wenye mechi mbili mkononi ambao wanaendelea kuongoza kwa kuwa na tofauti nzuri ya mabao ya kufunga na kufungwa.

Hata hivyo Southampton ilicheza pungufu kwa muda mrefu katika mchezo huo baada ya Alexandre Jankewitz kutolewa nje kwa kadi nyekundu dakika ya pili na Jan Bednarek pia zikiwa zimebakia dakika nne mechi hiyo kumalizika.

Mabao ya Manchester United katika mechi hiyo yalifungwa na Aaron Wan-Bissaka dakika ya 18, Marcus Rashford dakika ya 25, Bednarek aliyejifunga dakika ya 34, Edinson Cavani dakika ya 39, Anthony Martial aliyepachika magoli mawili dakika ya 69 na 90 na Scott McTominay dakika ya 71.

Nyota Bruno Fernandes alifunga bao dakika ya 87 kwa penalti na Dan James alikamilisha karamu hiyo dakika za lala salama.

Hicho ni kipigo cha pili kikubwa msimu huu kwa kikosi hicho cha The Saints kinachofundishwa na Kocha Ralph Hasenhuttl baada ya kufungwa idadi hiyo ya magoli na Leicester miezi 15 iliyopita.

United imeingia katika rekodi ya kupata ushindi mnono kwenye Ligi Kuu England, ikipata ushindi kama huu mwaka 1995 ilipokutana na Ipswich.

Hasenhuttl alianza mchezo huo kwa kuwatumia wachezaji wake waliokulia kwenye akademi ya timu hiyo wakiwamo Kayne Ramsay na Jankewitz.

# TUCHEL AMMWAGIA SIFA MOURINHO

**LONDON, England**

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel amemtaja Jose Mourinho 'ni mmoja kati ya makocha bora duniani', ikiwa zimebakia saa chache kabla hajakutana na Mreno huyo kwenye mechi ya Ligi Kuu England itakayochezwa leo usiku.

Kikosi cha Tuchel kinatarajia kukutana na Tottenham kwenye Uwanja wa Tottenham Hotspur ikiwa na nafasi ya kupanda kwenye msimamo wa ligi hiyo kama wataibuka na ushindi.

Timu hizo kila moja ina pointi 33, ingawa Chelsea imecheza mechi moja zaidi.

Mjerumani huyo ambaye alishinda mechi yake ya kwanza tangu aliporithi mikoba ya Frank Lampard alipocheza dhidi ya Burnley Jumapili iliyopita, amekiri Mourinho amemwacha mbali katika taaluma hiyo ya kufundisha.

Akizungumza kuhusu Mourinho katika mkutano na waandishi wa habari kuelekea mchezo wao wa leo, Tuchel alisema: 'Ni mechi kati ya Tottenham dhidi ya Chelsea, na si mimi dhidi ya Jose. Ninafuraha kuona ninashindana na timu iliyo imara, kikosi chenye wachezaji wazuri, wanaojiamini, wenye uzoefu na walio tayari kupambana.

'Unaweza kusema ni mtu anayenivutia? Kiukweli, nilipoanza kufundisha yeye tayari alikuwa mbali, ni kama nyota ndani ya dunia.

Mourinho, alishawahi kuiongoza The Blues kwa vipindi viwili tofauti kuanzia mwaka 2004 hadi 2007 na akarejea tena kati ya mwaka 2013 na 2015, na alikuwa akiiongoza Inter Milan wakati Tuchel akiajiriwa kwa mara ya kwanza na klabu kubwa ya inayoshiriki Bundesliga ya Mainz mwaka 2009.





# RONALDO AIWEKA JUVENTUS PAZURI

**TURIN, Italia**

MSHAMBULIAJI Cristiano Ronaldo alifunga mabao mawili na kuifanya Juventus iliyokuwa nyuma kupata ushindi wa mabao 2-1 katika mechi ya kwanza ya hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Coppa Italia dhidi ya Inter Milan.

Mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Argentina, Lautaro Martinez aliiongoza Inter kwa kufunga bao mapema baada ya kupiga shuti lililomshinda golikipa wa Juve, Gianluigi Buffon kudaka.

Mkongwe Buffon alikuwa akiichezea timu hiyo katika mechi ya 1,100.

Hata hivyo, Ashley Young alimfanyia faulo Juan Cuadrado na kumfanya Ronaldo afunge bao la kusawazisha la penalti kwa timu yake.

Baada ya mshambuliaji huyo raia wa Ureno kusawazisha, alitumia makosa ya safu ya ulinzi ya wapinzani wao kufunga bao la pili na la ushindi katika mchezo huo.

Matokeo hayo yalionekana kama ni ya kulipa kisasi kwa timu hiyo ambayo ilichapwa mabao 2-0 katika mchezo wa Serie A uliochezwa Januari mwaka huu.

Juventus, mabingwa hao mara 13 wa mashindano hayo watawakaribisha Inter Milan katika mchezo wa marudiano utakaochezwa Jumanne Februari 9, mwaka huu jijini Turin.

HABARI MICHEZO

# ULIMWENGU AFUNGUKA SIMBA ILIVYOPIGA HATUA

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Mtanzania Thomas Ulimwengu amesema anakiona kikosi cha Simba kipo katika kiwango kingine baada ya uongozi wa klabu hiyo kuandaa mashindano ya Simba Super Cup kwa mara ya kwanza mwaka huu.

Simba ilitwaa ubingwa wa mashindano hayo ikiwa na pointi nne baada ya kuifunga Al Hilal kutoka Sudan mabao 4-1 na kutoka sare ya bila kufungana na mabingwa hao wa zamani wa Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ulimwengu alisema kulingana na michuano ya kimataifa wanayoshiriki wanahitaji kupata maandalizi mazuri na kupitisha mechi za kirafiki walizocheza, zitawaweka kwenye nafasi nzuri kuelekea hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Ulimwengu alisema hatua ambayo wamefikia Simba ya kuwaalika TP Mazembe na Al Hilal ni kubwa na wanatakiwa kupongezwa kwa sababu wamezipatia timu zote mazoezi kwa wakati muafaka.

"Simba wanatakiwa kupewa pongezi kubwa, hii ni taswira ya timu yao imepiga hatua kubwa zaidi, ukizingatia zamani tunaona timu za Tanzania ambazo ni wawakilishi wa michuano ya kimataifa kutumia mechi za ligi tu kujiandaa, kushindwa kupata mechi za nguvu."

"Ila kwa Simba wamefanya jambo kubwa na kumpa nafasi kocha wao kuandaa timu ya kimataifa, lakini kwa upande wetu imetusaidia kujiandaa kwa ajili ya mechi zijazo za Ligi ya Mabingwa Afrika," alisema Ulimwengu.

Aliongeza michuano ya Simba Super Cup imeipa pia nchi heshima na yeye kama Mtanzania anajivunia kuona taifa lake limeanza kutimiza ndoto zao.

"Tunajivunia kuona wageni wanakuja Tanzania na kuona mambo makubwa, zamani tulionekana sisi ni wasindikizaji, lakini sasa tumeanza kutajwa kwenye mafanikio, Simba imeshaweka alama tofauti na ya kujivunia kwenye bara la Afrika, tuwapongeze kwa uamuzi waliochukua," Ulimwengu alisema.

Katika hatua ya makundi ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba imepangwa Kundi A ikiwa pamoja na AS Vita ya DRC, Al Ahly ya Misri na El Merreikh ya Sudan na itaanzia kampeni zake Mjini Lubumbashi ifikapo Februari 23, mwaka huu.

Kikosi cha Simba leo kinatarajia kushuka kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma kucheza mechi yake ya 'kiporo' dhidi ya Dodoma Jiji, halafu itarejea kuwavaa Azam FC Jumapili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.



Winga wa Simba, Luis Miquisson (kushoto), akipambana kuwania mpira dhidi ya mchezaji wa TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Joseph Ochaya katika mchezo wa Simba Super Cup uliochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam Jumapili iliyopita. Timu hizo zilitoka suluhu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Oppah afikiria kufunga mabao 35

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI nyota wa Simba Queens, Oppah Clement, amesema amedhamiria kupambana na kufunga mabao katika kila mechi ili kufikia malengo yake ya kutwaa kiatu cha dhahabu Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania msimu huu.

Oppah ameshafunga mabao 20 katika michezo 11 ya ligi hiyo akifungana na Fatuma Mustafa wa JKT Queens.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam juzi, Oppa alisema baada ya kumaliza mzunguko wa kwanza anajipanga kuendelea na kasi ile ile kwenye duru la pili la ligi hiyo.

Straika huyo alisema malengo yake ni kuhakikisha msimu huu anafunga mabao 35 au zaidi endapo atapata nafasi ya kucheza na kufikia malengo ya klabu hiyo.

"Malengo makubwa ni kuona timu inapata matokeo mazuri, ushindi ni furaha kwetu pamoja na mashabiki, kwa upande wangu nitapambana kufikia malengo ya kuwa mfungaji bora, nimedhamiria kufunga mabao 35 au zaidi ya hayo," alisema Oppah.

Oppah hivi Karibuni alifunga mabao saba wakati timu yake ya Simba Queens ikiibuka na ushindi wa mabao 11-1 dhidi ya TSC Queens, katika mchezo uliochezwa Uwanja wa Mo Simba Arena hapa jijini.

Matokeo hayo yaliifanya Simba Queens kufikisha pointi 29 na kukwea hadi nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania nyuma ya vinara Yanga Princess wenye pointi 31.

## Waziri Junior amkubali Bocco

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa Yanga, Waziri Junior amemtaja mshambuliaji wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, John Bocco ndiye mchezaji anayemvutia na anatamani siku moja wacheze timu moja.

Akizungumza na gazeti hili kwenye mahojiano jijini Dar es Salaam, Waziri ambaye amewahi kuzichezea klabu ya Toto African, Azam FC, Mbao FC alisema anamkubali sana mshambuliaji huyo kwa jinsi alivyo na uwezo mkubwa uwanjani, lakini mkarimu anapokuwa nje ya uwanja.

"Ninamkubali sana Bocco, namna anavyocheza mpira, nilitarajia kumwona kwa sasa akicheza nje ya nchi, lakini kila kitu Mungu huwa anapanga. Ni mchezaji bora Tanzania na nje ya uwanja ni mtu mkarimu ambaye anajali sana watu, mimi mwenyewe ni rafiki yangu na huwa tunaongea mengi sana," alisema Waziri.

Kwa upande wa wachezaji wa Yanga, straika huyo alimtaja mchezaji wake bora katika kikosi cha vinara hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara ni golikipa, Metacha Mnata.

"Anastahili kuwa mchezaji bora kwa sasa, ana uwezo mkubwa," aliongeza.

Waziri pia amezungumzia suala ya yeye kutolewa kwa mkopo ambalo lilikuwa likizungumzwa kabla ya kumalizika kwa dirisha dogo na kusema ni kweli kuna timu zilikuwa zinamhitaji.

"Ni kweli unajua kama huchezi kwenye timu hizi kubwa, kuna timu zitahitaji huduma yako. Kuna timu zilileta barua kunihitaji, lakini kocha (Cedrick Kaze), alikataa na kusema kuna kitu anakiona kwangu na akasema raundi ya pili itakuwa ngumu kwa hiyo naweza kusaidiana na wenzangu ili kuipa timu ubingwa badala ya kuondoka."

Straika huyo alisema kila kitu kinahitaji subira, hivyo wakati wake ukifika atacheza kwa kiwango kinachohitajika kwa sababu anafahamu Yanga inachotaka na si mchezaji anataka nini.

Mshambuliaji huyo amefunga bao moja tu ambalo ilikuwa katika ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya KMC katika mchezo wa Ligi Kuu Bara uliochezwa Oktoba 25, mwaka jana.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# JUVENTUS YAJITOSA KUMWANIA POGBA

Wakala wa kiungo huyo aweka wazi kwamba maisha yake ndani ya United...

**JUVENTUS, Italia**

VIGOGO wa Italia, Juventus wamefunguka kuhusu 'plan B' yao ya kumhitaji kiungo, Paul Pogba ambaye anatajwa kuwa mhimili ndani ya kikosi cha Manchester United.

Juventus inatakwa kuanza mchakato wa kumrejesha Pogba nchini Italia, lakini hatima ya mchezaji huyo itajulikana wakati mchezaji huyo atakapokuwa huru.

Klabu hiyo inatajwa kusubiri ni kiasi gani Manchester United inahitaji kulipwa ili kumuuza kiungo huyo kabla Pogba pia hajafanya uamuzi wa hatima yake.

Taarifa Italia zinasema klabu hiyo inahusishwa zaidi na mpango wa kumsajili Mfaransa huyo ambaye aliwahi kuichezea timu hiyo ya jijini Turin kwa muda wa miaka minne.

Wakala wa Pogba, Mino Raiola aliweka wazi kwamba muda wa kiungo huyo kuitumikia klabu ya Old Trafford "umekwisha" na tayari ameitaja Juventus ina nafasi ya kumnasa nyota huyo.

Mkataba wa United na mshindi huyo wa taji la Kombe la Dunia unatarajiwa kumalizika ifikapo mwakani na inamaana kwamba wanatakiwa kufanya uamuzi mgumu katika kipindi hiki cha majira ya joto mwaka huu.

Juventus wanajipanga kuhakikisha wanamrejesha Pogba kwenye Uwanja wa Allianz Stadium mwishoni mwa msimu huu na Mashetani Wekundu wanatakiwa kuweka wazi thamani ya kiungo huyo hivi karibuni, Calcio Mercato inaripoti.

Mwaka 2016, Juventus ilimuuza kiungo huyo kwa pauni milioni 89 na huenda ikamrejesha kama mchezaji huru endapo itashindwa kuweka dau linalowezekana katika majira ya mwaka huu.

## KWA UFUPI

**KOEMAN AMWAZA MESSI**

KOCHA wa Barcelona, Ronald Koeman amesema anaamini lakini hana uhakika kama mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Argentina, Lionel Messi atabakia katika klabu hiyo kwenye kipindi cha majira ya joto. ***(Athletic - subscription required)***

**NEYMAR, PSG SAFI**

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Brazil, Neymar, ambaye ana umri wa miaka 28, anajiandaa kusaini mkataba mpya wa miaka minne na mabingwa wa Ligi Kuu Ufaransa, Paris St-Germain. ***(Goal)***

**PSG WAMWOTA MESSI**

VIGOGO wa Ligi Kuu Ufaransa, PSG wameweka wazi wanatamani kuona Neymar anaungana na mshambuliaji mwenzake wa zamani wa Barcelona, Lionel Messi katika kikosi cha Parc des Princes. ***(Metro)***

**MBAPPE AJIPANGA**

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Kylian Mbappe, mwenye umri wa miaka 22 na ambaye mkataba wake na PSG unatarajiwa kumalizika ifikapo mwakani, anajipanga kufanya uamuzi kuhusiana na hatima yake. ***(ESPN)***

**DIALLO AMRITHI SANCHO**

MANCHESTER United imeamua kuachana na mpango wa kumwania mshambuliaji wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho (20), baada ya kuvutiwa na winga raia wa Ivory Coast, Amad Diallo ambaye alijiunga na timu hiyo akitokea Atalanta. ***(Sun)***

**HAALAND, KOUNDE SOKONI**

STRAIKA wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya Norway, Erling Braut Haaland (20) na beki wa Sevilla Mfaransa Jules Kounde ambaye ana umri wa miaka 22, wametajwa kuwindwa na Manchester United. ***(Express)***

**SPURS YAMBANIA ALLI**

MWENYEKITI wa Tottenham, Daniel Levy amezuia mchakato wa PSG kumsajili kiungo wa Timu ya Taifa ya England, Dele Alli (24), kwa sababu ya kikosi cha Spurs kimekumbwa na majeruhi mbalimbali na vilevile kimeshuka kiwango. ***(Telegraph)***

**HAKIMI AGOMBEWA EPL**

ARSENAL, Chelsea na Manchester City zimeonyesha nia ya kunasa saini ya beki wa kulia wa Inter Milan na Timu ya Taifa ya Morocco, Achraf Hakimi (22), katika kipindi cha majira ya joto. ***(Calciomercato - in Italian)***

**ARMSTRONG AITOSA CITY**

MSHAMBULIAJI chipukizi wa Timu ya Taifa ya Jamhuri ya Ireland, Sinclair Armstrong (17), ambaye anawindwa na Manchester City, Celtic na Crystal Palace, anajiandaa kusaini mkataba mpya na klabu inayoshiriki Championship, Queens Park Rangers. ***(TalkSport)***

**BALOGUN NJIA MOJA**

MSHAMBULIAJI wa Arsenal ambaye ni raia wa England, Folarin Balogun (19), anaongeza nguvu katika mkakati wake wa kuondoka katika klabu hiyo kama mchezaji huru ifikapo mwishoni mwa msimu huu. ***(Express)***

**VINICIUS KUUZWA**

REAL Madrid inajiandaa kumuuza mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Brazil, Vinicius Junior ambaye ana umri wa miaka 20 ifikapo majira ya joto. ***(AS - in Spanish)***

HABARI MICHEZO

# AZAM FC YARIDHISHWA SARE NA TP MAZEMBE

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kufanikiwa kuwabana mabingwa wa zamani wa Afrika, TP Mazembe, mabosi wa Azam FC wamesema wameridhishwa na kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wao kwenye mchezo wa kirafiki wa kimataifa uliochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, jijini Dar es Salaam juzi usiku.

Azam FC ilitoka sare ya bao 1-1 na TP Mazembe kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), katika mechi hiyo ya kirafiki ya kimataifa.

Ofisa Habari wa Azam FC, Thabit Zacharia, aliliambia gazeti hili licha ya kupata sare, lakini Kocha Mkuu wa timu yao, George Lwandamina, ameridhishwa na juhudi zilizoonyeshwa na wachezaji wake katika dakika zote 90 za mchezo huo.

Zacharia alisema mechi hiyo imewapata mazoezi mazuri wachezaji wao na imewasaidia kujiimarisha kuelekea mechi za lala salama za Ligi Kuu Tanzania Bara inayotarajiwa kuendelea kuanzia wiki ijayo.

"Matokeo hayakuwa kitu kikubwa. Alichofurahi kocha wetu ni jinsi wachezaji walivyofuata maelekezo yake, jinsi timu ilivyobadilika, hasa unapocheza na timu kama Mazembe wanaweza kukufanya ufanye makosa fulani ambayo huwezi kuona kwa timu za Tanzania zikikulazimisha kufanya makosa kama yale," alisema Zacharia.

Kiongozi huyo alisema Lwandamina ameridhishwa jinsi timu ilivyokuwa inajilinda, ikimiliki mpira na jinsi ilivyoshambulia.

Alisema baada ya mechi hiyo, timu yao itaendelea na mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mchezo dhidi ya mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba itakayochezwa Jumapili.

"Bado tuko kwenye mbio za ubingwa. Ubingwa uko wazi, ila cha muhimu ni kwamba tunataka tushinde mechi zetu. Kuna mechi nyingi zimebaki, ligi bado haijaisha, kwa hiyo chochote kinaweza kutokea," Zacharia alisema.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Azam yenye pointi 32 baada ya kucheza mechi 17 iko kwenye nafasi ya tatu, nyuma ya vinara Yanga yenye pointi 44 na Simba yenye pointi 35, lakini imecheza michezo mitatu pungufu.



Wachezaji wa KMC wakiwa katika mazoezi ya timu hiyo kwa ajili ya kujiandaa kuwakaribisha Namungo FC kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDANO**

# KMC, Namungo hapatoshi Uhuru

**Na Saada Akida**

MAKOCHA wa timu za KMC na Namungo FC kila mmoja ametamba kikosi kimejipanga kufanya vizuri katika mechi ya 'kiporo' ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Kocha Msaidizi wa KMC, Habibu Kondo, alisema anakiamini kikosi chake kiko imara kuelekea katika mchezo huo ili watimize malengo yao ya kumaliza kwenye nafasi za juu msimu huu.

Kondo alisema timu yake imefanya mazoezi kwa muda mrefu kwa sababu inafahamu ushindani huongezeka zaidi katika mechi za mzunguko wa pili.

"Tumejiapanga vizuri, kikosi chetu cha wana Kino Boys kimeshafanya maandalizi ya kutosha kuelekea katika mtanange huu, hatuna hofu kwa sababu viongozi na benchi zima la ufundi limejipanga vyema ili kuhakikisha alama tatu zinabaki nyumbani," alisema Kondo.

Aliongeza wanawaheshimu wapinzani wao lakini wanawataka wafahamu KMC FC ina timu nzuri na bora zaidi yao hivyo kila mmoja ajipange kupata matokeo yake.

"Kwa sasa kikosi cha KMC kimeimarika zaidi ikiwa ni baada ya kuongeza wachezaji wawili katika usajili wa dirisha dogo, ladha ya mpira kutoka kwa vijana wa Kinondoni inarudi katika safasi yake, tunawaomba mashabiki na wapenzi wa KMC wajiandae kupata ushindi, mechi za kirafiki tulizocheza zimetuimarisha," aliongeza kocha huyo.

Kocha wa Namungo, Hemed Morocco, aliliambia gazeti hili mechi zote za ligi ni ngumu, lakini amekuwa akiwakumbusha wachezaji wake kuongeza umakini.

Morocco alisema endapo watatumia vizuri nafasi watakazotengeneza, ushindi utakuwa ni wao katika mchezo huo.

## Kombe la FA Z'bar kumekucha

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MASHINDANO ya Kombe la Shirikisho la Zanzibar (ZFF) yamepangwa kufanyika kuanzia Februari 21, mwaka huu, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkurugenzi wa Mashindano wa ZFF, Ali Mohammed alisema michuano hiyo itashirikisha timu zote 12 zinazoshiriki Ligi Kuu Zanzibar, timu zote za Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja na Pemba.

Mohammed alisema timu nyingine ni kutoka katika ngazi ya Ligi Daraja la Pili Mikoa, ambapo kila moja itatakiwa kuwasilisha majina ya timu mbili ambazo zitashiriki michuano hiyo ambayo bingwa wake atapata tiketi ya kushiriki michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Alisema Kamati ya Mashindano imezitaka timu za madaraja ya chini kuanzia ngazi ya kanda na mikoa ambazo zitashiriki michuano hiyo kuzingatia vigezo vyote vinavyotakiwa ikiwamo kutumia wachezaji wenye leseni ili kuepusha usumbufu kwa klabu zitakazosonga mbele.

Alisema mashindano hayo yatachezwa kwa mfumo wa mtoano na kamati yake imejipanga vyema kuhakikisha hakuna vitendo vyovyote vya upangaji wa matokeo katika michuano hiyo.

## JKU yajitabiria mazuri Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya JKU imesema imejipanga vyema kuhakikisha inapata matokeo mazuri katika mechi za mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Zanzibar baada ya kufanyia kazi upungufu waliouona katika kikosi chao.

JKU imeendelea kujiimarisha katika mbio zake za kutwaa ubingwa wa ligi hiyo baada ya kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Chuoni katika mchezo wake wa raundi ya 11 uliochezwa kwenye Uwanja wa Amaan juzi.

Kocha Mkuu wa JKU, Omar Khamis, alisema licha ya mzunguko wa kwanza kutofanya vizuri, anaamini hali itakuwa tofauti katika mzunguko wa pili.

Khamisi alitaja moja ya upungufu ambao aliuona katika kikosi chake na kuufanyia kazi ni maboresho kwenye safu ya kiungo na ushambuliaji kwa kuongeza wachezaji wenye uwezo na uzoefu katika ligi hiyo.

"Tulikosa umakini katika nafasi nilizozitaja, hali hii ndio imesababisha kupoteza baadhi ya mechi huko nyuma na kupata matokeo mengi yasiyoridhisha, ninaamini tutarudi tukiwa imara zaidi," alisema Khamisi.

Aliongeza asilimia kubwa ya wachezaji wa Zanzibar viwango vyao na uchezaji wao unafanana, anaamini akipata wachezaji kutoka nje watasaidia kuziba pengo lililoko kwenye timu hiyo.

"Tulianza vibaya, lakini kadri tulivyokuwa tunacheza katika mzunguko huu timu yetu ilibadilika, tulianza kupata matokeo mazuri japo kwa kusuasua, lakini hapa tulipofikia sio tulikotoka, muhimu zaidi ni kuziba nafasi ambazo zina upungufu," alisema kiongozi huyo.

Michezo
Alhamisi Februari 4, 2021
Nipashe



## JUVENTUS YAJITOSA KUMWANIA POGBA

HABARI UK 22




Kikosi cha mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, benchi la ufundi na viongozi wa klabu hiyo wakiwa bungeni jana, baada ya kupata mwaliko maalumu ikiwa ni siku chache tangu walipotwaa kikombe cha mashindano ya Simba Super Cup 2021. **PICHA: MTANDAO**

## YANGA YAWATOA HOFU MASHABIKI

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI kukiwa na taharuki kuhusiana na adhabu ya kufungiwa kusajili kwa misimu mitatu, uongozi wa Yanga umesema dhamira yao kuu ni kuona timu zao mbili zinaibuka mabingwa katika msimu huu wa 2022/21 ambao umeingia katika hatua ya lala salama.

Yanga imekosa ubingwa wa Ligi Kuu Bara kwa misimu mitatu mfululizo wakati Yanga Princess inayoshiriki Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania haijawahi kutwaa taji hilo linaloshikiliwa na watani zao, Simba Queens.

Mwenyekiti wa Yanga, Dk. Mshindo Msolla aliliambia gazeti hili watakuwa na vikao baada ya kumalizika kwa kila mchezo kwa ajili ya kufanya tathmini na baadaye kujipanga na mechi inayofuata.

"Kila mwisho wa mchezo tutakaa kikao na benchi la ufundi ili kuwakumbusha makocha wa timu zote dhamira yetu ya kutwaa makombe," alisema kwa kifupi Msolla.

Ofisa Uhamasisha wa Yanga, Antonio Nugaz, alisema klabu yao itatoa ufafanuzi kuhusiana na hukumu ya kutosajili inayowakabili baada ya kuchelewa kumlipa mshambuliaji wake wa zamani, Amissi Tambwe.

"Tutatolea ufafanuzi kuhusu jambo hili, tunawaomba mashabiki wetu msiwe na wasiwasi, wadhamini wetu wapo, watalimaliza suala hili," Nugaz alisema.

# SIMBA, DODOMA JIJI HAPATOSHI

### Ni mechi ya kiporo ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo huku kila timu...

**Saada Akida na Agusta Njoji, DODOMA**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba wanatarajia kushuka ugenini kusaka pointi tatu muhimu dhidi ya wenyeji Dodoma Jiji FC katika mechi ya 'kiporo' ya ligi hiyo itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

Ligi hiyo ilisimama kwa muda kupisha Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), iliyokuwa inashiriki fainali za Kombe la Mataifa Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), kumaliza majukumu yake ya kimataifa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Simba, Suleiman Matola, alisema kikosi chao kiko tayari na kamili kwa mchezo huo ambao wanaamini hautakuwa mwepesi kwa upande wowote.

Matola alisema Simba imejiimarisha kila idara kuhakikisha wanapata ushindi katika mchezo huo na kuwakaribia watani zao, Yanga ambao wanaongoza kwenye msimamo wa ligi hiyo ya juu nchini.

Kocha huyo alisema watashuka uwanjani wakiwaheshimu wapinzani wao kwa sababu wanaamini wao pia wamejiandaa kuzibakisha pointi tatu za mchezo huo nyumbani ili watimize malengo yao.

"Tunamshukuru Mungu tumefika Dodoma salama, tunajua tulichokifuata huku ni pointi tatu, lakini hatuwezi kuzipata kama hatutapambana, ni wajibu wetu kuingia uwanjani kwa kujituma na kucheza kwa kiwango bora," alisema Matola.

Nahodha na kiungo huyo wa zamani wa Simba alisema wachezaji wote walioko jijini hapa wako salama na kila mmoja wao anafahamu wanatakiwa kupambana kusaka ushindi na si matokeo mengine.

"Tumekuja kupambana, tunajua ligi ilisimama na sisi tulikuwa katika mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika na bado tunaendelea, tunahitaji ushindi ili kuongeza hamasa kwenye timu kwa ajili ya kufanya vyema michezo mingine inayofuata," Matola aliongeza.

Mbwana Makata, Kocha Mkuu wa Dodoma Jiji aliliambia gazeti hili wamejiandaa kupambana na kuhakikisha 'wanaishangaza' Simba kwa kupata ushindi.

"Tumewaangalia Simba katika mechi zote walizocheza, tunajua ubora na upungufu wa kila mchezaji wao, naamini wachezaji wangu wakitekeleza vizuri maagizo na mbinu tulizowapa, tunaondoka na furaha baada ya dakika 90 kumalizika," alisema Makata.

Ofisa Habari wa Dodoma Jiji FC, Moses Mtanza, aliliambia gazeti hili wamejipanga na wamejiimarisha kuelekea mchezo huo ambao unasubiriwa kwa hamu na wadau mbalimbali wa soka hapa nchini.

"Tunakwenda kuchukua pointi tatu, iwe mchana, iwe usiku, kwa namna yoyote ile tunakwenda kuchukua pointi tatu, tunakwenda kumlewesha Simba, tunakwenda kula kiporo cha nyama ya Simba, hiki kiporo ni cha kwetu," alisema Mtanza.

**MNYAMA ALITEKA BUNGE**

Kikosi cha Wekundu wa Msimbazi jana, kilitinga bungeni huku wabunge wakitumia muda mrefu kuwashangilia wakati wakitambulishwa.

Mabingwa hao watetezi walitambulishwa bungeni katika kipindi cha maswali na majibu na Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson ambaye alisema ugeni huo una watu 34 ambao ni wachezaji, benchi la ufundi na viongozi mbalimbali wakiongozwa na Ofisa Mtendaji Mkuu, Barbara Gonzalez.

Kutokana na shangwe za wabunge, Dk. Tulia alilazimika kuwasimamisha kwa muda ili kukamilisha tangazo.

Akizungumza nje ya ukumbi wa bunge, Barbara alitamba timu hiyo itachukua ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu.

Barbara alisema Simba ina malengo makubwa ya kufanya vizuri katika mashindano ya ndani ya nchi na ya kimataifa wanayoshiriki.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002